# Nipashe

Alhamisi Mei 28, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580243

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Mchungaji adaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi, mapenzi na mama

UKURASA 2




UKURASA

# Madaktari washangaa maajabu ya 'nyungu' kupunguza corona



UKURASA 5







**KUSHOTO:** Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto) na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Ndogo na za Kati wa NMB, Filbert Mponzi (kulia), wakiwa wameshika alama ya uzinduzi wa akaunti ya NMB Pamoja kwa ajili ya vikundi vya kuweka na kukopa, jijini Dar es Salaam.
**KULIA:** Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kulia) na wakurugenzi wengine wa benki hiyo, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati wa Kongamano la Uwezeshaji Sekta ya Afya lililoandaliwa na CRDB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SABABU ZA IDRIS KUPEWA DHAMANA

UKURASA 2

# Vigogo Chadema kuhojiwa Takukuru

UKURASA 2

## BAA LA CORONA



Zingatia kunawa mikono kwa maji na sabuni na vitakasa mikono kila unapotoka nje ya mazingira ya nyumbani kwako kabla ya kushika kitu chochote hata mnyama unayemfuga. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



**MICHEZO** KAGERE KUPEWA 'DOZI' MAALUMU UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Vigogo Chadema kuchunguzwa

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema inachunguza tuhuma za ubadhirifu wa fedha dhidi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Uchunguzi huo unahusu fedha za michango ya kila mwezi inayotolewa na wabunge wa chama hicho kwa chama, ili kubaini kama kuna viashiria vya rushwa.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari (siyo Nipashe) jana, Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Bregedia Jenerali John Mbung'o, alisema michango hiyo inaratibiwa na chama hicho na hadi sasa wamewahoji baadhi ya wanachama waandamizi na viongozi mbalimbali.

Alitaja viongozi walioshahojiwa ni aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, ambaye kwa sasa ni mwanachama wa CCM, Dk. Vincent Mashinji.

"Tumeshakusanya nyaraka mbalimbali, tumeshawaita viongozi na wanachama waandamizi wa chama, tumeshamuita aliyekuwa Katibu Mkuu Mashinji, tumemuita mhasibu wao mkuu, tumeshapata nyaraka kutoka sehemu mbalimbali," alibainisha.

Aidha, Takukuru imewaita baadhi ya wabunge wa chama hicho kuchukua maelezo yao na kuwasiliana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhusiana na matumizi ya fedha za ruzuku ambazo chama hicho hupokea kila mwezi, lengo likiwa ni kuwianisha na michango hiyo ya wabunge hao.

Mkurugenzi huyo alisema uchunguzi huo unafanyika kufuatia malalamiko ya wabunge wa chama hicho kuhusu michango wakilalamikia kutokuwapo kwa uwazi wa matumizi ya fedha hizo, licha ya kuwa michango hiyo imeandikwa kwenye katiba ya chama hicho.

Ijumaa iliyopita, wabunge wawili wa viti maalum, Suzanne Masele na Joyce Sokombi, kutoka katika chama hicho walitangaza kukihama pamoja na mambo mengine, walitaja sababu iliyofanya waondoke ni kukosekana kwa uwazi kwenye matumizi ya fedha hizo.

Akifafanua michango hiyo, Mbunge Suzan Masele alisema wabunge wa viti maalum wamekuwa wakichangia chama hicho Sh. milioni 1.5 kila mwezi tangu Januari mwaka 2016 hadi Aprili 2019 kwa miezi 40, na kufanya jumla ya michango hiyo kufikia Sh. bilioni 2.2 ikiwa ni mchango wa Sh. milioni 62 kwa kila mbunge.

Mbunge huyo alidai kuwa suala hilo ni kwa mujibu wa katiba ya chama hicho, lakini kinachokosekana ni uwazi kwenye matumizi yake na hawaruhusiwi kuhoji kokote.



Msanii wa vichekesho Idrisa Sultani (kulia) na Innocent Maige, wakisubiri kusomewa mashitaka yanayowakabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mchungaji mbaroni madai kumpa mimba mwanafunzi

**Na Salome Kitomari**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Mlango wa Ukombozi Gairo mkoani Morogoro, Joseph Gervas (28), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa madai ya kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha tatu.

Pia, mchungaji huyo, mkazi wa kijiji cha Rubeho Kata ya Kisitwi, Tarafa ya Gairo, anadaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mama mzazi wa binti hiyo.

Akizungumza jana, Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchembe, alithibitisha kukamatwa kwa mchungaji huyo ambaye aliwaaminisha wanawake na mabinti kuwa kwa kufanya nao mapenzi anawatoa mapepo.

Alisema binti aliyepewa mimba alikuwa na matatizo ya macho, ndipo alipopelekwa kwa mchungaji huyo kwa ajili ya kuombewa. Alisema tatizo la macho lilisababisha kupata tatizo jingine la kuanguka na ndipo baba yake alimpeleka kwa mchungaji huyo kwa maombi.

Mchembe alisema mchungaji huyo aliishauri familia hiyo kumuacha binti huyo nyumbani kwake kwa siku kadhaa kwa ajili ya maombi zaidi, na ndipo alipoanza kumwingilia kimwili.

"Huko kwenye maombi kulikuwa na mabinti wengine wawili, ambao walikuwa wanafanyiwa hivi, lakini huyu mmoja ndiyo alikubali kusema wazi, alitaka kusema kabla, lakini mama yake alikuwa akimzuia," alisema na kuongeza:

"Mwanafunzi huyo aliamua kumweleza baba yake na baba alivyokuwa mkali kwa mama yake na binti ndipo mama wa binti alithibitisha kuwa na mahusiano na mchungaji huyo."

Alisema mchungaji huyo alikuwa akienda nyumbani kwa familia hiyo mara kwa mara wakati baba wa familia hayupo, na alikuwa akipikiwa vyakula kama nyama na chapati.

"Ndugu wa mume walishtushwa na mazoea hayo na walipofuatilia walibaini jambo na kumweleza ndugu yao (baba)," alisema.

"Kwa nyakati tofauti alikuwa anaenda kufanya maombi ya chumvi nyumbani kwa wahusika (wazazi wa binti), pia alikuwa anazungukia nyumba za watu hapo kijijini hasa wanawake," alisema.

Alisema: "Aliwaaminisha anatoa mapepo kwa kushiriki nao tendo la ndoa, wakati mwingine kuweka dawa kwenye sehemu zake za siri ndipo anawaingilia."

"Tulivyokuwa kwenye mkutano wa hadhara wanawake wengi walisimama na kuanza kueleza vitendo vya udhalilishaji walivyofanyiwa na mchungaji huyo kila walipokwenda kanisani kwake."

Alisema kuwa mtuhumiwa huyo anashikiwa siku ya tatu sasa, kwa ajili ya usalama wake kutokana na wananchi wa eneo hilo kuwa na hasira kiasi cha kutaka kumdhuru.


**MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LIMITED** tutauza kwa mnada wa hadhara Kiwanja cha mdaiwa sugu mali ya Ndugu Sylvia Yohana Sokazwe na Nyumba ya mdaiwa sugu Ndugu Veronica Waziri Lugongo dhamana zote zipo eneo la Kiwangwa –Kata ya Gabo -BAGAMOYO. Lengo ni kufidia / kupunguza madeni la mikopo wanayodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 06/06/2020 kuanzia saa nne asubuhi, mahali dhamana ilipo.

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:-**
**0757433333/0652113262/0717616227**

157506



**KUPOTEA KWA KADI**

**Enock Stephano Kalabwe** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki ainaya SANLG yenye namba za usajili T.754CWF Chasis No*LDAPAJOBXEC-BO3783*. Hivyo yeyote atakayeiona kadi hiyo apeleke taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Mjini Bariadi.

Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa katika kituo cha polisi cha Bariadi kwa namba **BAR/RB/1568/2015.**

157507


# Idris Sultan asomewa mashtaka mawili, apata dhamana

**Na Hellen Mwango**

HATIMAYE msanii Idris Sultan na mwenzake wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka mawili likiwamo kutumia kadi ya simu isiyokuwa na jina lake bila kutoa taarifa ya mtoa leseni, baada ya kusota polisi kwa siku saba.

Wiki iliyopita Idris alikamatwa na Jeshi la Polisi hadi jana alivyofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Mwandamizi, Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali Batilda Mushi na Estazia Wilson.

Mushi alidai kati ya Desemba Mosi 2019 na Mei 19, mwaka huu eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, Idris alitumia kadi ya simu ya mkononi namba 0753617621 mali ya Innocent Maiga.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitumia kadi yenye namba hiyo ya simu bila kutoa taarifa ya mtoa leseni.

Wilson alidai katika shtaka la pili, siku na tarehe za tukio la kwanza Maiga alishindwa kutoa taarifa ya mabadiliko ya umiliki wa kadi ya simu yenye namba 0753617621 kwa mtoa leseni.

Ilidaiwa Maiga alishindwa kutoa taarifa kwamba kadi hiyo inatumiwa na Idris. Washtakiwa walikana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, na kuomba mahakama tarehe ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali na haukuwa na pingamizi la dhamana.

Hakimu Chaungu aliwataka washtakiwa kuwa na wadhamini wawili kila mmoja watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 15 kila mdhamini.

Washtakiwa walitimiza masharti ya dhamana na wako nje mpaka Juni 9, mwaka huu watakaposomewa maelezo ya awali.

HABARI KITAIFA

## Vikundi vya kuweka, kukopa vyawezeshwa

**Na Enock Charles**

BENKI ya NMB imezindua akaunti maalum kwa ajili ya vikundi vya kuweka na kukopa hususani vya wanawake ili kutekeleza dhana ya kujiwekea akiba na kuwainua wananchi wa kipato cha chini kimaendeleo.

Lengo lingine ni kuepukana na upotevu wa fedha za vikundi ama kudhulumiana.

Katika taarifa ya benki hiyo kwa umma iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alielezwa kaunti hiyo inayojulikana kama 'NMB Pamoja Account' imeleta suluhisho kwani ni salama na inaondoa changamoto zote za fedha taslimu kama kudhulumiana na hata kuibiana michango ya wanachama.

"NMB Pamoja Account' ni akaunti maalum iliyotengenezwa kutoa huduma kwa mahitaji ya vikundi vya kijamii vilevile imetengenezwa kuangalia masuala ya ulinzi na hatari zinazohusiana na kuweka fedha majumbani," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mwanakikundi wa Pamoja Akaunti anaweza kutoa michango bila haja ya vikao, kuangalia salio, kuangalia taarifa fupi ya kifedha, kufungua akaunti ya kikundi ya benki kupitia mfumo wa kidijitali au simu janja au simu ya kawaida, kuhamisha fedha kutoka NMB Pamoja Akaunti ya kikundi kwenda akaunti binafsi za NMB bila makato yoyote.

Alisema akaunti hiyo pia inashirikiana na NMB ChapChap (akaunti ya papo hapo) kufanya miamala kati ya vikundi vyenye akaunti nyingine, na kwamba ushirikiano huo utasaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma za NMB na bidhaa zake kwa karibu zaidi, kwa wateja na wasio wateja wa benki hiyo hasa walio vijijini na wa vipato vya chini.

Zaipuna alisema kupitia huduma hiyo, wateja wanapata ahueni kwa kutumia simu za mkononi kama njia ya kisasa, huku ikiwapunguzia adha ya kupeleka fedha taslimu ya kikundi benki na pia ya kuhudhuria vikao mbalimbali vya vikundi.

## Kesi ya Mbunge yapigwa kalenda

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SHAURI namba 10 la mwaka 2020 la uhujumu uchumi, linalomkabili Mbunge wa Jimbo la Kishapu, mkoani hapa, Suleiman Nchambi (CCM), limeahirishwa hadi Juni 25, mwaka huu, litakapotajwa tena.

Kesi hiyo ilitajwa katika Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ushindi Swalo, kutokana na upelelezi kutokamilika. Mei 13, mwaka huu, Wakili wa mshtakiwa, Frank Mwalongo, aliwasilisha hati ya maombi ya dhamana dhidi ya mteja wake katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, kutokana na Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na utoaji wa dhamana kiasi kisichozidi Sh. milioni 10.

Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Shinyanga, Phocus Mkeha, alisema mbunge huyo ana haki ya kupewa dhamana kwa masharti ya kusaini bondi ya Sh. milioni 50 na mdhamini wake bondi ya Sh. milioni 10 pamoja na kushikiliwa pasipoti yake ya kusafiria.

Alisema maamuzi ya utoaji wa dhamana hiyo ameyarudisha katika Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga, kesi yake ya msingi ilipoanzia na watasimamia masharti ya utoaji wa dhamana hiyo. Hata hivyo, maamuzi ya hatima ya dhamana ya mbunge huyo ilikuwa ijulikane Mei 11, mwaka huu, katika Mahakama ya Wilaya, lakini iliahirishwa hadi Mei 25, mwaka huu kutokana na Jumatatu kuwa sikukuu na mshtakiwa kuwa nje kwa dhamana.

# Saut yazindua dawati la unyanyasaji kijinsia

**Na Rose Jacob, MWANZA**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ameutaka uongozi wa Chuo Kikuu cha Saut, kuhakikisha dawati la kutatua changamoto za kijamii chuoni hapo halitumiki vibaya ili kuleta mstakabali ndani ya jamii.

Alitoa rai hiyo wakati akizindua dawati hilo, jana, katika chuo hicho kwa kushirikiana na Tahiliso.

Chuo hicho kimekuwa cha kwanza Tanzania kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilolitoa Agosti 9, mwaka jana, la kutaka vyuo vyote nchini kuunda madawati ya kushughulikia changamoto vyuoni hasa unyanyasaji wa kijinsia.

"Suala la kutatua changamoto ndani ya vyuo na kijamii zinaihitaji weledi mkubwa ili kuleta usawa na kumaliza tatizo ili mambo yaende vizuri, na washauri mumtangulize Mungu katika kusikiliza mashauri hayo," alisema Mongella.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo cha Saut, Balozi Prof. Costa Mahalu, alisema kutokana na mwingiliano wa shughuli za kijamii ni vigumu kuzikwepa changamoto mbalimbali za kijamii kwa kiwango kikubwa zikiwamo watu kunyimwa haki ya kusikilizwa, unyanyasaji wa kijinsia, mikopo ya wanafunzi, migogoro na migogano, anuwai baina ya wanajamii.

"Tumeanzisha dawati hili ambalo litashughulikia matatizo mbalimbali ya wana Saut katika mahusiano yao hususani, wanafunzi kwa wanafunzi, wafunafunzi kwa wahadhiri, watoa huduma, watumishi wa utawala wa chuo, watumishi wa taasisi zilizopo ndani ya Saut, wanajamii wanaokizunguka chuo na nina imani chuo kufanikiwa," alisema Prof. Mahalu.



# Shahidi adai kushuhudia unga mweupe mbele ya Nsembo

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI Kelvin Charles (22), amedai mahakamani alishuhudia unga mweupe na wa njano ukifungwa mbele ya Abdul Nsembo (45) na mke wake Shamim Mwasha (41), katika bahasha tano tofauti.

Kadhalika, alidai kuwa baada ya bahasha hizo kufungwa yeye pamoja na washtakiwa wote wawili waliandika majina yao matatu na kutia saini.

Ushahidi huo dhidi ya kesi ya Uhujumu Uchumi namba 4/2020, umesikilizwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama mafisadi iliyoketi chini ya Jaji Elinaza Luvanda.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Constantine Kakula, shahidi alidai kuwa anafanyakazi katika kampuni ya usafi ya Kishingweni kama mfanyausafi.

Alidai kuwa Mei 2, mwaka huu saa 2:00 asubuhi akiwa anaendelea na kazi ya usafi nje ya jengo la Utumishi Kivukoni, jijini Dar es Salaam, alifuatwa na mwanamke.

"Nikiwa nafanya usafi nilifuatwa na Inspekta Johari akanieleza kwamba anamuhitaji kwenda kushuhudia ufungaji wa vielelezo kwenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, alikubali alikwenda ofisini kwake akawakuta washtakiwa wote wawili Nsembo na Mwasha," alidai na kuongeza.

"Alileta vielelezo vikiwa pamoja akaviweka pamoja mezani, nilishuhudia akiviwekea alama moja mpaka tano na A mpaka E, mimi na washtakiwa wote tuliandika majina yetu na tulitia saini juu ya bahasha zote tano," alidai Charles.

Alidai kuwa anawatambua washtakiwa wote kwa sababu alitambulishwa siku alipoitwa na Inspekta Johari kwenda kwenye ofisi zao kwa ajili ya ushahidi huru.

Akihojiwa na mawakili wa utetezi, Nassoro Juma, shahidi alidai kuwa siku ya tukio aliwaona washtakiwa kwa macho na kwamba ulifanyika utambulisho.

Alidai kuwa hajawahi kutoa ushahidi dhidi ya watuhumiwa katika mamlaka hiyo.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kusafirisha dawa hizo za kulevya, Mei mosi, mwaka huu wakiwa eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam kinyume na sheria ya uhujumu uchumi.



Sehemu ya jengo lenye maduka ya biashara likiwa limedondoka katika eneo la Salasala, jijini Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa mashuhuda, ukuta huo uliporomoka wenyewe bila kuguswa na chochote na kujeruhi watu watatu. **PICHA: SALOME KITOMARI**

# Mkutano Baraza la Mawaziri Sadc waanza

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc) umefanyika jana kwa njia ya mtandao, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC).

Mkutano huo ulifunguliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maofisa Waandamizi/Makatibu Wakuu, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Wajumbe wengine waliohudhuria ni Katibu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, pamoja na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipago, Amina Shaaban.

Mkutano wa Baraza la Mawaziri utafanyika kesho baada ya kukamilika kwa kikao cha kamati hiyo ambayo imejadili masuala mbalimbali ndani ya jumuiya ikiwamo mlipuko wa virusi vya corona ndani ya SADC.

Mkutano huo utaangalia utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Baraza la Mawaziri kilichofanyika mwezi Aprili 2020 kuhusu Covid-19 na athari zake katika utekelezaji wa programu za SADC, athari za kijamii na kiuchumi na madhara yake ndani ya jumuiya.

Pia, mkutano huo umejadili hali ya kifedha ndani ya jumuiya, utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na kikao cha Baraza la Mawaziri wa SADC ambayo ni Menejimenti ya Maafa, utekelezaji wa kaulimbiu ya Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC isemayo "Mazingira Wezeshi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya Viwanda, Kukuza Biashara na Ajira ndani ya SADC" na mapitio ya hali halisi ya biashara baina ya nchi, maendeleo ya viwanda ndani ya jumuiya na taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Jumuiya na Mpango kazi wake.

Mkutano huo umehusisha wataalamu kutoka nchi wanachama 12 wa SADC sekta za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Fedha na Mipango, Uchukuzi na Mawasiliano, Viwanda na Biashara, Maliasili na Utalii pamoja na Afya.

## UFUPI

### Bil. 34/- zapeleka maendeleo Kilolo

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Aloyce Kwezi, amesema halmashauri hiyo inajivunia kasi kubwa ya utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo kutokana na jitihada zilizofanywa na Rais John Magufuli za kutoa fedha za utekelezaji wa miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 34.2.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kwezi alisema miradi hiyo ya kimaendeleo imeifanya halmashauri hiyo wananchi wake waipende serikali zaidi kwa kuwa miradi mingi imejibu malalamiko ya kero zao.

"Tunautambua mchango mkubwa wa Rais wetu mpendwa Dk. Magufuli, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Waziri wa Tamisemi ambao wamesukuma kasi ya maendeleo katika Halmashauri ya Kilolo na sasa tunapofunga mwaka tuna miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo ni heshima kubwa kwa Kilolo," alisema.

Pia, halmashauri hiyo imeendelea kutekeleza mradi wa mfereji wa Mgambalenga unaojengwa kwa Sh. bilioni 21 kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wanaojishughulisha na kilimo cha umwagiliaji.

Alisema kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya imetoa Sh. milioni 76, wakati Japan kupitia Shirika lake la JICA imejitolea fedha zinazosalia katika mradi huo.

### Wajasiriamali wapewa mil. 50/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wamepewa fursa ya kunufaika na Sh. milioni 50 zolizotolewa na Benki ya Stanbic.

Utoaji wa fedha hizo ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 25, benki hiyo Tanzania, baada ya kuzindua shindano la wajasiriamali kwa lengo la kuchochea ukuaji wa shughuli za kibiashara nchini.

Shindano hilo liitwalo, 'Stanbic Entrepreneurship Challenge' linatarajiwa kuanza leo hadi Juni 11, mwaka huu, ambapo washindi watano watazawadiwa Sh. milioni 10 kila mmoja.

"Nchini Tanzania, sekta ya biashara ina kampuni ya biashara ndogondogo na za kati (SMEs) zaidi ya milioni 3, ambazo zinamchango mkubwa katika kukuza na kuimarisha uchumi. Na kwa kuwa ni dhumuni letu kuu ni kuhakikisha kwamba sekta hii inakuwa, kwa miaka mingi tumekuwa tukiendesha programu ambazo zimeweza kuwanufaisha wajasiriamali kupitia mafunzo, kuwaunganisha wataalamu wa biashara na kuwaandalia madarasa na wakufunzi sekta ya biashara," alisema Mkuu wa Idara ya Masoko wa benki ya Stanbic, Desideria Mwegelo.

Alisema shindano hilo linawalenga wafanyabiashara ambao wanaweka jitihada kubwa kuhakikisha wanafikia malengo yao kupitia miradi inayoleta manufaa ya kijamii, kwenye sekta za afya, elimu, mazingira, teknolojia, pamoja na shughuli za uzalishaji na chakula.

# MAT yashangaa maajabu nyungu kupunguza corona

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT) kimesema kinafanya uchambuzi ili kubaini tiba mbadala ambazo zimetumika kwenye kukabiliana na virusi vya corona zina mchango gani katika kupungua kwa maradhi hayo Tanzania.

Rais wa chama hicho, Dk. Elisha Osati, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati MAT ikitoa tathmini ya kitaaluma kuhusu mwenendo wa corona.

Dk. Osati alisema tathmini waliyoifanya kuhusu mwenendo wa corona, wamebaini idadi ya wagonjwa imepungua kwa kiasi kikubwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma wakiwamo wanaohitaji kuwekewa oksijeni.

"Tunafanya uchambuzi ambao tutautoa unaolenga kujua kitu gani kimechangia na kwa namna gani kimepunguza corona Tanzania.

"Hatuwezi kudharau njia mbadala kwa sababu Watanzania wengi wanatumia miti shamba, wengi walikuwa wanatumia limao, tangawizi ambavyo vina vitamin C kwa wingi inayosaidia kujenga kinga ya mwili ili kupambana na wadudu mbalimbali wakiwamo corona."

Alisema inawezekana tiba mbadala imekuwa na nafasi yake, hivyo uchambuzi kuhusu hilo utakuja.

"Watanzania tumewaelekeza vitu vingi vya kufanya watu wananawa mikono, wiki tatu mfululizo watu wamevaa barakoa, tunaamini hiyo imesaidia kupunguza tatizo pia. Kila kimoja tutakifanyia uchambuzi ikiwa ni pamoja matumizi ya tangawizi na limao," alisema.

Akizungumza ugonjwa huo, Dk. Osati alisema Aprili sampuli zilizokuwa zikipelekwa maabara takribani 90 zilikuwa na corona wakati kwa sasa ni chini ya asilimia 10.

"Idadi ndani ya jamii zimepungua, kwa kuangalia idadi ya simu zinazopigwa kwa kuuliza au kuomba msaada wa kitaalamu kuhusu wagonjwa wenye dalili za ugonjwa huu. Pia idadi ya vifo imepungua," alisema.

Alisema MAT kimempongeza Rais John Magufuli, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu kwa kuwaongoza Watanzania katika kipindi hicho kigumu.

"Tunawapongeza madaktari na watumishi wa sekta ya afya kwa kuwa askari wa mbele kupambana na corona.

"Tunawaomba wagonjwa walioko nyumbani kwa matatizo ya corona au magonjwa mengine waje hospitali tuwahudumie, kwani corona imepungua kwa kiasi kikubwa. Madaktari tupo tayari kuwahudumia."

Chama hicho kimewaeleza Watanzania kuwa ugonjwa huo bado upo, hivyo waendelee kuchukua tahadhari hasa wakati huu wa wanafunzi wanaporudi vyuoni.

Naye, Rais Mteule wa MAT, Dk. Shadrack Mwaibambe, akielezea tangawizi alisema ina madini ya Zinc kwa wingi ambayo yanasaidia katika ukuaji wa seli na kuiongezea nguvu.

"Kama corona wanashambulia seli zinazokuongezea kinga mwilini na madini haya ya Zinc yakaiongezea nguvu hiyo seli ni wazi mwili wako unaweza kuwa na kinga ya kupambana na virusi.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (kulia), akikabidhi vifaa vya kujikinga na kudhibiti maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19, ambavyo ni vitakasa mikono, barakoa, matangi ya maji, mabeseni na ndoo kwa wawakilishi wa shule na vyuo vilivyopo mkoani humo jana, ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha sita na ualimu. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Waliotafuna mabilioni ya Pride kufikishwa kortini

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema watu waliojimilikisha viwanja, kula fedha zilizokuwa za Kampuni ya Pride Tanzania, watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Waziri Mpango aliyasema hayo bungeni wakati akitolea ufafanuzi wa hoja zilizoibuliwa na wabunge wakati wakichangia taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2018/19.

Wabunge hao walitaka majibu ya serikali juu ya kampuni hiyo kudaiwa Sh. bilioni 130.149 zikiwa ni za mikopo kwa taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi, amana za wateja, malipo ya bima na watoa huduma wengine.

Pia walilamika kuwapo kwa ubadhirifu wa Sh. milioni 585.935 za malipo ya watoa huduma mbalimbali kwa huduma ambazo hazikufanyika katika kampuni hiyo kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka 2017.

"Mheshimiwa Spika, tumehangaika sana sana na Kampuni ya Pride kama serikali, kwa kipindi kirefu imekuwa ikiendeshwa kinyemela kama kampuni binafsi mpaka Oktoba 2018, ndipo Mahakama Kuu ya Tanzania kupitia Division ya Biashara ndipo ilipotoa uamuzi wa makubaliano kuwa Pride ni mali ya serikali," alisema Dk. Mpango na kuongeza:

"Pamoja na hatua ambazo serikali imezifanya kuitwaa rasmi Pride, lakini tulihitaji kuhakiki mali na madeni ya Pride na kazi hii imefanyika na imekamilika, serikali hiyo hiyo, ilimwagiza CAG kufanya ukaguzi maalumu ili kuiwezesha kufanya maamuzi yanayostahili," alisema Dk. Mpango.

Dk. Mpango aliongeza: "Na niliambie Bunge lako tukufu, ukaguzi huo umekamilika na tunaendelea kuichambua hiyo taarifa, ili tuweze kuchukua hatua sahihi ili kuboresha utendaji wa Pride, timu ya wataalamu ndani ya serikali imeundwa na inaendelea na kazi ya kuchambua."

Alisema: "Mheshimiwa Spika nikuhakikishie kabisa, pamoja na bunge lako kwamba wale wote waliojimilikisha Pride wakala fedha za umma, wakachukua na viwanja hawa tutawashughulikia kwa mujibu wa sheria za nchi."

Kuhusu Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kufanya operesheni ya maduka ya kubadilishia fedha iliyofanyika mwaka 2018, Dk. Mpango alisema: "Mpaka sasa bado maduka 10 tu ambayo mchakato unaendelea, wakimaliza majadiliano watarudishwa vifaa vyao tukishajiridhisha tuko sawa, shughuli zao zinaendana na maslahi ya taifa."

# Mfumo kudhibiti wabunge watoro

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

SPIKA Job Ndugai amesema katika kuimarisha mahudhurio ya wabunge bungeni pamoja na ulinzi, umefungwa mfumo maalum wa utambuzi kwa wabunge watakaokuwa wanaingia ndani ya viwanja vya Bunge.

Amesema mfumo huo utaweza kumtambua mbunge kwa sura tofauti na sasa wanapoweka saini kwa alama ya dole gumba.

Aliyasema hayo juzi bungeni kabla ya kuahirisha vikao vya bunge na kueleza kuwa Bunge limeshafunga mfumo huo ambao utatambua wabunge waliohudhuria na watu walioingia bungeni.

"Unajua mambo ya ku-log in kumekuwa na changamoto zake, hata hivyo katika kuimarisha mifumo bungeni, umefungwa mfumo mpya wa Facial, kwenye kila mlango wa bunge hivyo siku zijazo hakutakuwa na changamoto kwa wabunge ambao hawahudhurii," alisema Ndugai.

Mbali na taarifa hiyo, Spika Ndugai aliwataka wabunge kutopeleka maombi ya msamaha wa kodi ya magari kwa sababu mchakato huo ulishamalizika muda wake na mfumo kufungwa.

"Kama kuna wabunge wanaomba msamaha wa kodi kwenye magari wanayoagiza, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wamelijulisha Bunge kuwa muda wa kufanya hivyo umeisha na mfumo umefungwa," alisema Ndugai na kuongeza:

"Hivyo msituletee tena maombi hayo, tumalizie muda uliobaki vizuri maana ni mdogo, msituletee maombi ya msamaha wa kodi ya magari, tusubiri kuomba kura kama mtarudi mtaanza nayo kuanzia Novemba," alisema Spika Ndugai.

YEYE SIYO MKOROFI

Aidha, Spika Ndugai aliwaeleza wabunge kuwa yeye siyo mgomvi kama watu wanavyodhani, na kwamba huwa mkorofi hadi mtu amchokoze kwa makusudi.

Kauli hiyo aliitoa wakati akimsifia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, kutokana na kazi nzuri anayofanya tofauti na aliyepita.

"Awali kulikuwa na mambo ya kudharauliana, na kwa bahati nzuri mbivu na mbichi zimeonekana na haiwezekani kuwapo watu wa ovyo ovyo.

"Ni sehemu ya miaka mitano, lakini kelele, uongo mwingi kwa kuwa mwisho wa siku lazima Bunge liheshimiwe... watu wengine hawanifahamu vizuri, mimi siyo mgomvi ukiona naparangana na mtu ujue kanichokoza, ukifanya hivyo makusudi utaona," alisema Spika Ndugai.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Chereko sera ijayo ya ajira*

HAPANA shaka ni jambo linaloigusa umma katika sura pana kupitia tamko, sera mpya ya ajira iko jikoni na ndani ya muda mfupi ujao itawekwa hadharani.

Ujumbe huo rasmi unatoka kinywani kwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, alipohojiwa kwenye televisheni juzi, akitaja sababu kuu ni kuitaka iendane na uhalisia wa mazingira ya sasa.

Ipo wazi kwamba kuna mabadiliko mengi yamefanyika katika uhalisi wa maisha, tangu sera iliyoko ilipoanza kutumika miaka 12 iliyopita.

Pia, ni tamko linalogusa furaha ya umma wa waajiriwa, ambao nao katika tasfiri pana ni kuanza na waliowaajiri, wengine wengi walio karibu nao, ama ndugu na rafiki au wadau wa karibu wa nyendo za utumishi huo, pasipo kuwasahau waliojiajiri na kuajiriwa katika mifumo isiyo rasmi.

Vivyo hivyo, kuna kundi kubwa la walioko katika mifumo rasmi ya kusaka ujuzi na maarifa, ama katika hatua ya nyongeza au mara ya kwanza, ambao baada ya kupumzishwa nyumbani kwa msukosuko wa corona, tena wanaitwa madarasani katika vyuo vyao, wageni nao wanakaribishwa.

Alisema wapo katika hatua za mwisho za kubadili sera ya ajira, iliandikwa zamani mwaka 2008 na haiendani na maisha ya sasa kwa sababu kuna mabadiliko makubwa ambayo yametokea katikati hapa.

Kwa mujubu wa Mavunde, wunataka kutengeneza sera ya ajira ambayo itaendana na mazingira ya dunia ya leo. Kama tunavyojua ajira ni shughuli yoyote halali inayomwingizia mtu kipato.

Kimsingi, ujumbe wa Mavunde unaibua lingine lijaloiwajibisha umma, kudadisi kwa kina maana ya sera, ambayo kamusi inaipatia tafsiri rahisi; utaratibu wa kuendesha jambo, ili kukidhi haja ya serikali.

Kuzaliwa sera mpya ya ajira, inatarajiwa kuwa na nyenzo inayobeba mtazamo wa aina fulani kutoa majibu ya kitaifa kwamba ni namna gani kilio cha ukosefu wa ajira kinapatiwa ufumbuzi.

Pia, kuna matarajio ya majibu namna mchakato wa ajira utaendana na matakwa halisi, hali kadhalika matarajio ya kitaifa leo na kesho.

Vivyo hivyo kwa waliioajiriwa, inabeba dhana namna watatimiza kilichowaingiza kazini, wakati huo huo wakikabiliana na changamoto za mageuzi yanayojitokeza huko walikoajiriwa.

Matakwa ya Taifa yanajulikana kuwa na asili ya kutegemeana. Mathalan, kunapaswa kuwapo uhusiano wa moja kwa moja kati ya sera za elimu, ajira na mifumo ya uchumi, bila ya kusahau nyendo za uongozi kitaifa.

Kuna ukweli kwamba, kupitia sera na maamuzi makuu ya kitaifa, zimezaa hatua kuu zinazobebana na mwelekeo wa nchi, vyote vikiegemea msimamo mkuu wa siasa za nchi.

Ikirejewa darasa la historia ya nchi, ni kwamba muda mfupi baada ya Muungano mwaka 1964, kulizaliwa siasa mpya na sera nyingi zikazaliwa baada ya hapo, hata kuibua mikakati mingi ya kitaifa, ikiwamo Mpango Mkuu wa Maendeleo wa Mwaka 1964 - 1969 ambao ndio mzizi mkuu wa mengi kiuchumi.

Utekelezaji wake ulizaa mengi, mathalan Azimio la Arusha ya Mwaka 1967, iliyomilikisha njia kuu za uchumi kitaifa kuwa za umma, hata ukalazimisha mageuzi makuu ya usimamizi na utendaji wa katika ofisi za umma, sheria zake, pia kuzaa shirika la kusimamia utumishi wa mashirika ya umma - Scopo.

Kwa maana hiyo, Sera ya Ajira iliyoko jikoni, ina tafsiri pana kuliko sentensi fupi aliyoitamka Naibu Waziri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Neema mpya ya madereva wetu kujihami na corona

HIVI karibuni serikali iliwataka madereva wa malori nchini kuchukua tahadhari dhidi ya mambukizo ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa corona, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanakula vyakula vitakavyolinda kinga zao za mwili.

Rai hiyo imetolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJW), Ummy Mwalimu, wakati akizungumza na baadhi ya madereva wa kampuni mbalimbali za malori zinazosafirisha mizigo nje ya nchi waliofika katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, iliyoko Mabibo jijini Dar es Salam, kwa ajili ya kupima kama wana maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona au la.

Waziri Ummy anasema ugonjwa wa corona bado upo, ingawa ukweli wa upande wa pili ni kwamba maambukizo yamepungua.

Jambo muhimu hapo ni kwa wananchi kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya. Hiyo inajumuisha kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, kunawa mikono kwa sabuni na majisafi yanayotiririka, kuvaa barakoa, pia kukaa umbali wa zaidi ya mita moja kati ya mtu na mwingine.

"Nimefurahi sana kuwaona mko hapa kwa ajili ya kupima virusi vya corona, kama mtakutwa hamna maambukizo ya ugonjwa huu mjitahidi kula matunda yakiwamo machungwa, mananasi, malimau, mboga za majani na tangawizi.

"Hii itawasaidia kinga zenu za mwili kuwa juu. Pia muwapo safarini mnapopata nafasi msisahau kupiga nyungu," anasema Waziri Ummy.

Kaimu Mkurugenzi wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, Ambele Mwafulango, anasema pamoja na kupima vipimo vya wagonjwa wengine kwa upande wa madereva walioko jijini Dar es Salaam, kwa siku wanawapima madereva 200 walioko mikoani na kuna utaratibu maalum wa kuchukuliwa sampuli zinazotumwa Dar es Salaam kwa ajili ya vipimo.

> **"Katika maabara hii ya Mabibo, tuna mashine mpya tano ambazo ndani ya saa 24 zinapima vipimo 1,800 hii imetufanya kupima vipimo vingi zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa katika maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko ofisi za NIMR jijini Dar es Salaam.**

Majibu ya vipimo hivyo yanatoka baada ya saa 48 kama madereva hao watakutwa hawana maambukizo na watapewa vyeti vinavyotumika kwa siku 14, itakayowasaidia kwenda kupeleka mizigo nje ya nchi, bila ya kupimwa tena katika nchi wanazokwenda.

Mwafulango anasema kabla madereva hao hawajafanyiwa vipimo vya corona, wanapimwa joto la mwili na wale ambao watakutwa na joto la juu la mwili watapewa huduma ya haraka zaidi ukilinganisha na wale ambao joto lao la mwili liko sawa.

"Madereva ambao tunawakuta hawana maambukizo ya ugonjwa wa corona tunawapa elimu ya kujikinga na ugonjwa huu wanapokuwa safarini siku zote.

"Katika maabara hii ya Mabibo, tuna mashine mpya tano ambazo ndani ya saa 24 zinapima vipimo 1,800 hii imetufanya kupima vipimo vingi zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa katika maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko ofisi za NIMR jijini Dar es Salaam.

"Tulikuwa na mashine mbili ambazo zilikuwa zinapima vipimo 300 hadi 400, jambo lililokuwa linachelewesha utendaji wetu wa kazi," alisema Mwafulango.

Serikali imetenga utaratibu maalum kwa ajili ya madereva wa malori wanaosafirisha mizigo nje ya nchi ambao wanafanyiwa vipimo vya ugonjwa wa corona kabla ya kusafiri, ili kuhakikisha hawana maambukizo na kuwaepusha kupata usumbufu ambao utajitokeza wanapokuwa safarini.

# TANGAZO

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

### TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA FBME BANK LIMITED (ILIYO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa iliyokuwa FBME BANK LIMITED kwamba;

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 51.77% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia ya bima ya amana, kufika kwenye yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

**MKURUGENZI**
**DEPOSIT INSURANCE BOARD**
**JENGO LA MAKAO MAKUU YA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**
**2 MTAA WA MIRAMBO**
**GHOROFA YA 11,**
**MNARA WA KASKAZINI**
**11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ**
**SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390**
**Fax: +255 22 223 4200**

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

### TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA MBINGA COMMUNITY BANK PLC, COVENANT BANK FOR WOMEN (T) LTD, EFATHA BANK LTD, KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LIMITED, MERU COMMUNITY BANK NA NJOMBE COMMUNITY BANK LIMITED (ZILIZO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa zilizokuwa;

1. **Mbinga Community Bank Plc,**
2. **Covenant Bank for Women (T) Ltd,**
3. **Efatha Bank Ltd,**
4. **Kagera Farmers Cooperative Bank Limited,**
5. **Meru Community Bank Limited na**
6. **Njombe Community Bank Limited, kwamba;**

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia matawi yote ya benki ya TPB Bank Plc yaliyopo nchini.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 37.91% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia zao kufika kwenye tawi lolote la benki ya TPB Bank Plc ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

**MKURUGENZI**
**DEPOSIT INSURANCE BOARD**
**JENGO LA MAKAO MAKUU YA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**
**2 MTAA WA MIRAMBO**
**GHOROFA YA 11,**
**MNARA WA KASKAZINI**
**11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ**
**SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390**
**Fax: +255 22 223 4200**

# Chadema yaukosoa utaratibu kupitisha maadili uchaguzi 2020

**Na Romana Mallya**

WAKATI Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ikitoa fursa ya siku moja kwa vyama vya siasa kujadili na kupitisha maadili ya Uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimeikosoa hatua hiyo.

Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, alisema haiwezekani itengwe siku moja kujadili na kuisaini bila kutoa muda kufanya marekebisho kama yapo.

"Sheria ilivyo, tume imeweka kwenye maadili haya kifungu ambacho kinatulazimisha hata kama hayapo sawasawa lazima kuyasaini.

"Ni kitu ambacho kimsingi hakikubaliki, lakini kwa sababu wameshakiweka na kama mlivyoona ratiba ya leo ni ya vyama kujadili na kusaini, tutafanya hivyo."

Alisema tafsiri yake ni kwamba tume imeshafanya uamuzi na leo wameitwa kujadili na kusaini.

Mnyika alisema Chadema itasaini, lakini haimaanishi wanakubaliana na mambo mengine ambayo hayafai kwenye maadili hayo.

Katibu Mkuu wa Chama cha Democratic Party (DP), Abdul Mluya, alisema awali walipatwa na mshtuko kwa nini wajadili na kusaini, lakini wamebaini hakuna vitu vipya kilichobaidilika ni mpangilio ndio umebadilika hivyo hawaoni sababu ya kutokusaini.

Mkurugenzi wa Haki za Binadamu na Sheria wa Chama cha Wananchi (CUF), Salvatory Magafu, alisema: "Rasimu ipo vizuri na tunakwenda kuipitisha kwa kanuni, kuna mambo mazuri, lakini kuwapo kwa mambo mazuri ni jambo moja na kuyasimamia ni jambo lingine, tunaipitisha iwe kanuni hivyo zinapaswa kusimamiwa kwa maslahi ya wadau wote wa uchaguzi."

Naye, Mwanasheria wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Ernest Makunga, alisema rasimu hiyo inakwenda kutengeneza maadili ya uchaguzi ya rais, wabunge na madiwani na itaweka mazingira bora ya kufanya uchaguzi kuanzia kampeni hadi mwisho.

Mwenyekiti wa NEC, Jaji Rufani mstaafu Semistocles Kaijage, alisema maadili hayo yanapaswa kufuatwa kwa lengo la kudumisha amani ya nchi na kuwa na uchaguzi huru na wa haki.

"Tume imejidhatiti na imejipanda kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba, sheria na kanuni pamoja na kuzingatia masharti ya kanuni za maadili ya uchaguzi," alisema.

Alisema wanaamini serikali, viongozi wa siasa, na wagombea binafsi wataheshimu maadili hayo na kuhamasisha wanachama wao kuyaheshimu.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, alisema rasimu hiyo imelenga kutatua changamoto zilizojitokeza kwenye uchaguzi wa mwaka 2015 katika uchaguzi mkuu na zile ndogo zilizofuata baadae.

"Nec ilipitia maoni hayo na kuyafanyika kazi, vyama vitatu ambavyo ni NCCR Mageuzi, Chadema na Alliance for Democratic Change (ADC) viliwasilisha maoni kwa kuchelewa kiasi kwamba tume ilikuwa imeshaleta kwenu barua ya mwaliko wa kikao hiki cha leo," alisema.

Alivitaja vyama vilivyowasilisha maoni yao kwa wakati Nec ni DP, Tadea, CUF, CCM, CCK, AFP, UPDP, UMD na Chauma.



Wachuuzi wakiwa wamepanga bidhaa zao chini kwenye Barabara ya Uhuru katika eneo la Ilala, jijini Dar es Salaam jana, na kusababisha usumbufu kwa waenda kwa miguu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mikakati kupokea wanafunzi kwa tahadhari corona yaanza

**Na Waandishi wetu**

SHULE mbalimbali zimeanza maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha sita, kwa tahadhari kubwa ya kukabiliana na corona.

Wilaya zilizotangaza maandalizi hayo ni Moshi, Hai, Monduli na mkoani Mwanza.

Wilayani Monduli, viongozi na watendaji wameanza maandalizi yaliyofanyika ni kuweka miundombinu ya kuwawezesha wanafunzi kuchukua tahadhari watakaporejea shuleni.

Ofisa Elimu wa Wilaya ya Monduli, Theresia Kiyara, alisema mengine ni kukusanya baadhi ya vifaa zikiwamo ndoo za maji, vitakasa mikono, pamoja na mafunzo kwa walimu.

"Sisi kama idara ya elimu tunaunga mkono jitihada za Serikali kupambana na corona, tumejiwekea mikakati mbalimbali ambayo tumeigawanya kwa awamu tatu, awamu ya kwanza ni kutoa vifaa kwa walimu katika ofisi zote awamu ya pili ni kutoa elimu ya afya kwa walimu kutoa elimu ya corona kila asubuhi shule zitakapofunguliwa," alibainisha.

Kwa mujibu wa Kiyara, awamu ya tatu itakuwa kuwashirikisha wadau wakiwamo wazazi kuhakikisha wanafunzi wote wanapata barakoa, ndoo na sabuni na maeneo ambayo yana changamoto za maji wanapata vitakasa mikono.

**RC ATAKA MAZOEZI**

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amewataka wakuu wa shule na vyuo kuhakikisha wanafunzi wanafanya mazoezi na maombi wanaporudi shuleni ili kuwajengea uimara kwa kuwa vita ya kukabiliana na corona.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na maofisa elimu, wakurugenzi, wakuu wa shule, wakuu wa chuo na maofisa mbalimbali wa mkoa huo kwenye ufunguzi wa mapokezi ya wanafunzi wa vyuo na kidato cha sita, kuwa wakati huu ni wa kuwa pamoja kuwasimamia watoto kwa kuwa corona ipo, lakini maisha lazima yaendelee.

"Mimi walinipima Aprili 27, mwaka huu majibu yalipokuja Aprili 30 nilikuwa na corona, lakini nimeushinda ugonjwa kwa kufanya mazoezi, kupiga nyungu na dawa za michanganyiko baadaye nikapima tena nikawa 'negative' ukweli maneno ya Rais yameniponya... hivyo Watanzania tufanye kazi tusibweteke, Rais anatusihi wakati wote, lakini muhimu ni kuzingatia maelekezo ya Wizara ya afya," alisema Mongella.

Aliongeza kuwa ofisi ya mkoa imeamua kukabidhi vifaa vya kujikinga na kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo ambavyo ni sanitizer, barakoa na seti za kunawia mikono ambayo ni matangi ya lita 200, mabeseni na ndoo kwa shule na vyuo vilivyopo mkoani humo. Nicholaus Magige, Mkuu wa Chuo cha Ualimu Butimba na Castory Mazula, Mkuu wa Shule ya Sekondari Messa, walisema baada ya kupata maelekezo, wamejipanga katika hatua za awali bila kuathiri matatizo ya kiafya na kuondoa msongamano kwa kuwatawanya wanafunzi kukaa mbalimbali pia kwenye bweni.

Kadhalika, upimwaji wa mara kwa mara utafanywa kwa kila wanafunzi na watumishi.

**DC: AWAONYA WANASIASA**

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amewatuhumu baadhi ya wanasiasa kwamba wanahujumu maelekezo ya serikali kuwarejesha shuleni wanafunzi wa kidato cha sita na kujiandaa na mitihani ya taifa.

Aliwataka wakuu wa shule ambao wanafunzi wa kidato cha sita watashindwa kuripoti shuleni katika muda uliopangwa, waende ofisini kwake Juni 2, mwaka huu.

Jana, Ole Sabaya alieleza kuhusu mkakati huo wa baadhi ya wanasiasa, wakati alipokutana na wakuu wa shule 10 za sekondari za kidato cha tano na sita wa wilaya hiyo, wakuu wa vyuo viwili, wataalamu wa afya, wakuu wa idara za Halmashauri ya Wilaya ya Hai na viongozi wa dini.

***Imeandikwa na Asraji Mvungi (MONDULI), Godfrey Mushi (HAI) na Neema Emmanuel (MWANZA)***


NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA AGIZO LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Februari mwaka huu lilitolewa Agizo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Taasisi zote za Umma, Wizara na Idara za Serikali na wakala za serikali zinazodaiwa malimbikizo ya kodi ya pango na Shirika la Nyumba la Taifa ziwe zimeshalipa madeni yao kabla au ifikapo Mei 30, 2020.

Tunapenda kuzishukuru Taasisi, Idara na Wizara zilizotimiza wajibu wao kwa kulipa kodi na malimbikizo wanayodaiwa. Hata hivyo, zipo taasisi kadhaa ambazo hazijatimiza wajibu wao wa kulipa kodi na malimbikizo yao wanayodaiwa na Shirika. Tunapenda kuzihimiza taasisi ambazo hazijatekeleza Agizo la Serikali zijitahidi kulipa madeni yao kabla Shirika halijawasilisha taarifa rasmi ya ulipaji wa madeni kwa Mamlaka kwa hatua stahili.

Lipa kodi yako ili tujenge Taifa letu

LIMETOLEWA NA:

OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA
NA HUDUMA KWA JAMII NHC- MAKAO MAKUU

157535

# Diwani alia na tembo waharibifu mazao

**Na Julieth Mkireri, BAGAMOYO**

DIWANI wa Kiwangwa, Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo, Malota Kwaga, ameiomba serikali kupitia kitengo cha wanyamapori kufika katika kata hiyo kudhibiti tembo wanaoharibu mazao ya wananchi.

Akiongea na waandishi wa habari juzi Lugoba, katika Halmashauri ya Chalinze, Malota alisema, tembo hao wamevamia katika mashamba ya wakulima na kuharibu mazao.

Alisema, wanatokea katika Hifadhi ya Saadani na kuharibu mahindi, mpunga, na sasa wameanza kuhamia kwenye mashamba ya mananasi jambo ambalo ni la hatari kwa wakulima.

"Tunaomba watu wa wanyamapori wafike kuwafukuza hawa tembo ambao wanasababisha hofu ya njaa kwa siku zijazo kutokana na mazao yao waliyopanda kuharibika," alisema Malota.

Alisema mashamba yaliyoharibiwa ni katika maeneo ya Minazi, Misani na pembezoni mwa mto Wami yalipo mashamba mengi ya wananchi. Malota alisema, tembo hao kuvamia mashamba ya wakulima ni jambo la kujirudia kila mwaka ambalo husababisha hasara kwa wakulima.



Mwasisi wa mradi wa kusaidia makundi yanayoishi katika mazingira magumu ya Masks for Hope, Bernice Fernandes (wa tatu kushoto), akitoa elimu kwa mamalishe na babalishe wa soko la Tegeta Nyuki, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa kampeni ya kupambana na maambukizo ya corona, sambamba na kugawa barakoa 1,000 kwa mamalishe hao, bodaboda, bajaji na yatima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi zatakiwa ushirikiano uratibu uchimbaji mchanga

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limependekeza kushirikiana na halmashauri, wasimamizi wa mabonde na kamisheni ya madini kushirikana kuandaa mwongozo wa uchimbaji endelevu wa mchanga katika mito.

Pendekezo hilo limetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alipotembelea eneo la Matosa, Wilaya ya Ubungo unakopita Mto Mbezi. Ziara hiyo imesaidia watumishi wa NEMC kujionea hali ya mazingira na madaraja ilivyo kufuatia mvua zilizonyesha jijini Dar es Salaam.

Aliwahamasisha vijana wanaochimba mchanga kujiunga katika vikundi ili wapewe utaratibu wa kufanya shughuli ya uchimbaji endelevu.

"Tukiweka utaratibu wa pamoja tutaweza kutengeneza ajira kwa vijana na pia halmashauri zitakusanya mapato," alisema na kuongeza kwamba mazingira yatatunzwa iwapo kutakuwapo utaratibu unaofanya uchimbaji wa mchanga kuwa endelevu.

"Tayari Mkuu wa Mkoa ametoa waraka kwa halmashauri zote kushirikiana na NEMC na Wizara ya Madini kuandaa mpango endelevu wa uchimbaji wa mchanga katika mito ya mkoa wa Dar es Salaam," alisema Dk. Gwamaka.

Ameeleza kuwa mito hujaa maji kutokana na uchafu na mchanga kuziba njia za mito na kisha kusababisha miundombinu kuharibika, na kuongeza kwamba uchimbaji mchanga ukiratibiwa, uharibifu wa miundombinu na mafuriko vitapungua.

"Ni muhimu kulinda miundombinu ya serikali ambayo inagharimu kiasi kikubwa cha fedha za walipakodi. Hivyo lazima kuwe na utaratibu utakaofanya vijana kuchimba mchanga kwa namna endelevu," alisema Dk. Gwamaka.

Aliwataka vijana kuunda vikundi ili watambuliwe na serikali za mitaa yao ili pindi mwongozo ukitoka wapatiwe vibali vya kufanya uchimbaji ulio endelevu na kuwapo urahisi wa kuwafuatilia.

"Hatua hii itapunguza gharama kwa serikali ya kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibika," alisema Dk. Gwamaka.

Vijana wachimbaji wamweleza Mkurugenzi Mkuu huyo kuwa kazi yao inasaidia kupunguza mafuriko kwa maelezo kwamba wakisafisha maeneo maji hupita kwa urahisi na kwamba changamoto yao kubwa ni vibali vya kufanya shughuli hiyo.

Jeremia Kitomari, aliomba serikali kutoa vibali vya kuchimba mchanga katika mito, na kueleza kwamba shughuli yao inasaidia kuondoa uchafu kwenye mito na kurudisha kina cha mto katika hali yake halisi.

"Licha ya kwamba tunapata kipato kupitia uchimbaji mchanga kwenye eneo hili nakulifanyia usafi, mara kwa mara tumekuwa tukikamatwa kwa kukosa kibali. Tunaomba mtusaidie," alisema Kitomari.

## Wanafunzi kilimo wapewa fursa SBL

**Na Enock Charles**

WANAFUNZI wanaosomea masomo ya kilimo katika vyuo mbalimbali vinavyofundisha masomo hayo nchini, wamehakikishiwa kuendelea kupatiwa ufadhili wa masomo.

Wamepewa uhakika huo na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa kueleza kuwa itaendelea na programu yake ya kutoa ufadhili kwa inayojulikana kama Kilimo Viwanda Scholarship.

Hatua hii ya SBL inakuja baada ya serikali kutangaza kuwa vyuo vyote vitafunguliwa kuanzia Juni Mosi, mwaka huu kutokana na kupungua kwa maambukizo ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu au Covid-19.

Taarifa ya jana ilisema imeshakamilisha makubaliano na vyuo viwili zaidi kimoja cha Iringa na kingine cha Kagera ambapo jumla ya wanafunzi 20 kutoka vyuo hivyo viwili watanufaika na ufadhili huo wa masomo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL John Wanayancha, vyuo viwili ambavyo ni Kaole Wazazi College of Agriculture cha Bagamoyo mkoani Pwani na Kilacha Agriculture and Livestock Training Center cha Moshi mkoani Kilimanjaro vimeshaingia makubaliano na kampuni hiyo na wanafunzi 20 wananufaika na ufadhili wa masomo.

Programu ya Kilimo Viwanda Scholarship inawalenga wanafunzi kutoka katika jamii za wakulima zenye vipato duni na ambazo haziwezi kuwalipia ada watoto wao. Kupitia programu hii, jumla ya wanafunzi 40 watakuwa wakinufaika na ufadhili wa masomo kila mwaka.

"Tunaamini programu hii itasaidia kuongeza wataalamu wa kilimo nchini ambao ni nguzo muhimu ya kuwasaidia wakulima kuongeza tija katika uzalishaji, hivyo kuwasaidia kuongeza kipato chao," alisema Wanyancha.

Aliongeza kuwa programu hiyo ni sehemu ya mkakati wa kampuni hiyo wa kuongeza kiasi cha nafaka ambacho kampuni hiyo inanunua kwa ajili ya uzalishaji wa bia ambazo ni pamoja na mahindi, shayiri na mtama. Alisema, mwaka jana ilinunua zaidi ya tani za ujazo 17,000 za nafaka kutoka kwa wakulima wa ndani sawa na asilimia 70 ya mahitaji yake yote ya malighafi kwa mwaka.

"Kampuni inalengo la kuongeza kiasi cha malighafi inayonunua kutoka kwa wakulima wa ndani hadi asilimia 85 kufikia mwaka 2020 na ndiyo maana tumeona umuhimu wa kusaidia kusomesha wataalamu wa kilimo ili wakafanye kazi ya kuboresha kilimo chetu. Kwa sasa kampuni inanunua malighafi kutoka kwenye mtandao wenye wakulima 400 nchini," alisema.

## Mdee ahoji mradi wa viwanja 20,000

MBUNGE wa Kawe (Chadema), Halima Mdee, amehoji utekelezwaji wa mradi wa viwanja 20,000 ambao Wizara ya Ardhi iliuza viwanja kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema katika Jimbo la Kawe mradi huo ulitekelezwa katika kata za Mbweni na Bunju.

Mdee alisema wananchi walilipia viwanja kwa maelekezo kwamba gharama za viwanja zingetumika kuboresha miundombinu mbalimbali katika eneo husika.

"Lakini ahadi hiyo haikutekelezwa kwa ufasaha, hali inayosababisha kero kubwa ya mafuriko na kutuama kwa maji hususan kipindi cha mvua, kero kubwa ikiwa ni Mtaa wa Mbweni Teta na Mbweni Malindi. Je, ni lini serikali itatatua kero hii?" Alihoji.

Katika majibu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilikiri kuwa kati ya mwaka 2003 na 2008 serikali ilitekeleza mradi wa upimaji viwanja hivyo.

Ilisema maeneo hayo ni pamoja na Bunju, Mivumoni, Mbweni JKT na Mbweni Malindi katika Manispaa ya Kinondoni.

"Jukumu la wizara lilikuwa ni kufungua barabara kwa mujibu wa michoro ya mipango miji na upimaji, baada ya barabara hizo kufunguliwa zilikabidhiwa katika halmashauri husika ambako viwanja hivyo vipo ili waziendeleze zaidi na kuzihudumia," ilisema.

Aidha, ilisema ni wajibu wa serikali kuhakikisha kuwa mitaa ambayo viwanja hivyo vimepimwa inapitika wakati wote ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

"Kwa sasa serikali imeanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini ambapo mamlaka hiyo imeendelea kutekeleza zoezi la urekebishaji wa miundombinu kwa maeneo yanayohitajika," ilisema.

Ilitolea mfano kazi inayoendelea katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni katika viwanja vya mradi katika eneo la mwongozo.

"Wajibu wa serikali ni kuwaonyesha watekelezaji ramani za viwanja ili kuweka miundombinu kuendana na mpango," ilisema.




Habari na Augusta Njoji

# Idadi ya watu wenye ulemavu walioteuliwa serikalini yatajwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



BUNGE limeelezwa kuwa kati ya watumishi 2,859 wenye ulemavu waliopo katika mfumo wa taarifa za kiutumishi na mshahara, watumishi 46 wameteuliwa kushika nafasi mbalimbali za kiuteuzi.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Amina Mollel (pichani).

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kwa mujibu wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma wenye ulemavu imeelezwa bayana umuhimu wa kukusanya na kutunza takwimu za watu wenye ulemavu katika utumishi wa umma.

"Je, mpaka kufikia sasa kuna watu wenye ulemavu wangapi kwa kuzingatia aina zao za ulemavu ambao wana ajira katika utumishi wa umma?" Alihoji.

Pia alihoji kati ya watumishi hao wangapi ambao wamepata fursa ya kuteuliwa katika nafasi mbalimbali za kiuteuzi.

Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na serikali mwaka 2005, ilibainika kuwa pamoja na mambo mengine haukuwapo utaratibu wa kukusanya na kutunza takwimu za watu wenye ulemavu katika utumishi wa umma.

"Kufuatia changamoto hiyo, mwaka 2012 serikali iliamua kuingiza kipengele cha kuwatambua watumishi wake wenye ulemavu kwenye Mfumo wake wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara na hivyo kuiwezesha kuwa na takwimu sahihi za watumishi wenye ulemavu," ilisema.

Aidha, ilisema kwa mujibu wa Takwimu za mwaka 2007, watu wenye ulemavu waliokuwa wameajiriwa katika Utumishi wa Umma walikuwa 689.

Hata hivyo, ilisema hadi kufikia Agosti, 2019 kulikuwa na watumishi 2,900 wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

"Kati ya watumishi hao, watumishi 2,859 wamo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mshahara na watumishi 41 wako nje ya mfumo," ilisema.

Ilieleza kuwa takwimu hizo zinaonyesha kuwa serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa katika kuongeza idadi ya watumishi wenye ulemavu katika utumishi wa umma ili kuwapa nafasi katika ujenzi wa Taifa kupitia ajira zao.

# Uvunaji mamba waundiwa kikosi kazi

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeunda kikosi kazi cha kufanya tathmini ya kina ili kuainisha idadi ya mamba watakaovunwa nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwamo Ziwa Ilamba katika Wilaya ya Busokelo.



Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Busokelo (CCM), Fredy Mwakibete (pichani).

Katika swali lake, mbunge huyo alisema Ziwa Ilamba limekuwa na mamba wengi na wananchi wengi wamepoteza maisha na wengine kujeruhiwa na mamba hao.

"Je, ni lini serikali itawavuna mamba hao ili wananchi wa maeneo yanayozunguka ziwa hilo waishi kwa amani?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema pia serikali za vijiji na wilaya zinashauriwa kujenga uzio maeneo ambayo shughuli za kibinadamu kama kuoga, kuchota maji na kufua zinafanyika ili kuepusha wananchi kupata madhara yanayosababishwa na mamba.

Ilisema matarajio ya wizara ni kuwa tathmini itakapokamilika, uvunaji kwa njia ya minada utafanyika ili kupunguza adha kwa wananchi.

Ilifafanua kuwa wizara inatambua changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini hususani mamba.

"Kutokana na changamoto hiyo, wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kunusuru maisha ya wananchi ikiwa ni pamoja na kushughulikia matukio yanayohusu mamba kwa haraka iwezekanavyo pindi yanapojitokeza," ilisema.

Kufuatia hali hiyo, ilisema wizara imeunda kikosi hicho ili kujua idadi za mamba hao.

ama
ALHAMISI MEI 28, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Wenye ualbino: Tunatimiza miaka 40 yenye ushindi mkuu**


Ukurasa 13

Kisa saratani; umaskini unaua wenye ualbino wengi ujanani


Ukurasa 14

**Waziri Ummy: Ndivyo ilivyo shida iliyosumbua upimaji Covid – 19**

AFYA

NGUVU YA UTAMADUNI...

# Matazamio China na mitishamba ya corona yashuhudia mbadala

**Na Nimi Mweta**

KUIBUKA aina mbalimbali za mitishamba nchini na kwingineko barani Afrika, ikiwa sehemu ya ubunifu kupambana na janga corona, kumebadili upepo wa mchepuo mpya wa biashara ya China ilikokuwa inatazama.

Ni matumizi ya dawa za asili kutibu viashiria vya corona, kwani wataalamu wanakubaliana kuwa endapo inashambuliwa mapema, inatibika kwa haraka zaidi, ila ikikomaa inakuwa 'shughuli.'

China ilishaanza kujipanga kutafuta masoko kutokana na mafanikio katika kupambana na kasi ya maambukizo na vifo kutoka maradhi ya corona.

Ni hali iliyowezesha kueleweka katika baadhi ya maeneo ambayo ni ya kimataifa na kitaifa, yanayoendana na utamaduni na uzoefu wa tiba wa nchi.

Juhudi za China zina wenzake barani Afrika, kwani si muda mrefu, Rais Andry Rajoelina wa Madagascar, alifungua kwa kutangaza ugunduzi wa dawa inayotibu virusi vya corona.

Baadhi ya jumuiya za vyombo vya habari na nyenzo za kimataifa, zimeipa utambulisho kama nguvu nyepesi kwa matamshi 'herbal tea' hivyo kubebesha dhana ni 'kitu laini'na siyo 'dawa kamili'.

Kinyume chake, ina mtazamo wa nchi kadhaa za Afrika kuchangamkia wazo au bidhaa hiyo ya Madagascar; Tanzania ilishatuma ndege kuchukua shehena ya bidhaa hiyo, ambayo iko mikononi mwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa za Binadamu (NIMR), kwa uhakiki.




Mzigo wa dawa ya corona, kutoka nchini Madagascar. **PICHA: MTANDAO.**

> **China ilishaanza kujipanga kutafuta masoko kutokana...**

Pia, kuna sababu inayojitokeza kisaikolojia kuwa Madagascar ni Waafrika wenzetu, hivyo dawa zinazokubalika kwao hata sisi zitatufaa.

Waziri mwenye dhamana na Uhusiano wa Kimataifa, Prof. Palamagamba Kabudi, alipokea shehena akiwa na waziri mwenzake wa Madagascar, walioonekana wakiinywa, kwa kubeba maana kwamba haina madhara katika hatua hiyo ya mwanzo

Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) halijatamka kuipa uthibitisho, sambamba na dawa nyinginezo duniani kudaiwa kugundulika.

Katika mengine yanayohusiana na ugunduzi wa kienyeji yanajumuisha matumizi ya jamii au mimea kama malimau, majani na matunda katika sura ya kujikinga,. vilevile tiba.

Ina maana kwamba aina za mimea, majani, mboga au matunda yanayofaa kutumia kujikinga au kuondoa viashiria vya corona, inategemea mahali mtu alipo na ushauri anaopata, ambayo ni kama kusema ni mwendelezo wa tiba za kienyeji, si ushawisi kutoka nje.

Kilichoko katika jamii ya Kitanzania, kuna sura ya ya kuchangamkia bidhaa hiyo ya Madagascar, ikizingatia ina wasifu 'haina madhara'kuna ubaya gani kujiwekea kinga?

Ina maana, tiba mbadala za China zina saikolojia ya kuenezwa zaidi katika jamii ambako utamaduni wa China umeshika.

Hapo ieleweke kwamba, kuna raia wengi wa China wameenea duniani hasa katika sekta ya ujenzi na miundombinu kwa jumla, hivyo kuna nafasi ya wao na 'wafuasi' kusikiliza wataalamu kuhusu hizo tiba mbadala.

Cha kukumbukwa, ni kwamba kuna mazoea na utamaduni wa Wachina wanapoweka kambi ya kikazi mahali fulani wakiwa na wenyeji, wana mazoea ya uhusiano wa kawaida uliozama na si ajabu 'kuchotwa' katika tiba za Kiafrika.

Kwa hali hiyo, hata raia wa China walioko nje ya kwao hawatoi uhakika wa mitishamba ya kwao kuwa na nafasi ugenini, kwa wao kuwa wakala wazuri.

Ushiriki wao katika mazingira ya kawaida na shughuli za kila siku za vijiweni, maeneo ya ujenzi au baa, ni ishara tosha utamaduni kama vile lugha wanazotumia na mengi yanayoambatana, pia huelekezwa kule wenyeji wanakoangalia, si ajabu tiba ikawemo.

Hapo, Wachina kuchangamkia tiba za ugenini, kuna wakala mashiko ya kiutamaduni, inayomuidhinisha mtumiaji kukubali kisaikolojia.

AFYA

# Wenye ualbino: Tz tunatimiza miaka 40 yenye ushindi mkuu

• Sensa ya Taifa imewahesabu • Shida kwenye kodi mafuta yao • Walia wakunga kuwananga wajawazito




Katibu wa Chama Cha Watu Wenye Ualbino (TAS), akiwa na mwanachama wake na mdau mkuu wa haki za kinamama, Christine Silas. **PICHA: KHADIJA KALILI**

**Na Khadija Kalili**

IFIKAPO Juni 13 mwaka huu Chama Cha Watu Wenye Ualbino nchini (TAS) kinatazamia kutimiza miaka 40 tangu kuasisiwa, huku kikiingia umri kwa kishindo cha mafanikio katika malengo iliyojiwekea.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Katibu Mkuu wa TAS, Mussa Kabimba, anataja wanachojivunia kuwa ni kuwapo ongezeko la huduma za afya zinazopewa watu wenye ualbino.

"Chama kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine, tumefanikiwa kuboresha na kuimarisha upatikanaji tiba ya awali ya saratani ya ngozi kwa mikoa saba Tanzania Bara na Visiwa vya Zanzibar.

"Hiyo inatokana na ushawishi mkubwa uliotolewa na chama chetu TAS kwa serikali, kuanza kununua mafuta ya kupunguza mionzi ya jua (sun screen lotion) kwa kupitia Taasisi ya Saratani Ocean Road na baadhi ya halmashauri za wilaya nchini," anasema Kabimba.

"Chama chetu kilianzishwa mwaka 1978 na kusajiliwa rasmi mwaka 1980, ambayo kilikuwa na lengo la kuwaunganisha watu wenye ualbino na kutetea haki na maslahi yao ya kielimu, afya na ustawi wao, ili kuondokana na dhana potofu kuhusu ualbino kwenye mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania," anaeleza.

Kabimba anasema TAS, kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine, wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza ukatili utokanayo na imani za kishirikina, akiamini ni ishara ya mafanikio

> **Maelekezo ya mafuta hayo mwenye ualbino yeyote atakayeyatumia, anatakiwa akae kwenye eneo ambalo halina jua, ila kutokana na ugumu wa maisha na kutafuta riziki wengine (wenye ualbino) hupaka na kisha kuingia mtaani.**

Anaongeza, mauaji nayo hivi sasa yamepunguzwa nchini kwa kiwango kikubwa, ikiwa ni majivuno ya ushirikiano kutoka serikalini na wadau wengine, hata ikatengwa Siku ya Kitaifa ya Kuongeza Uelewa Kuhusu Ualbino, ikiwa na ushawishi mkubwa.

Pia, Kabimba anatumia vielelezo vya maendeleo kwao kama vile Rais Dk. John Magufuli, kutambua uwezo na vipawa vyao, hata kuwaingiza katika historia ya Bara la Mawaziri, akieleza: "Uteuzi huu kwa wenzetu albino inatoa hamasa kwa kizazi kilichopo na kijacho."

### CHANGAMOTO JE?

Katibu huyo anataja changamoto yao, ni ugumu wa kupatikana, pia kufikiwa huduma hizo za kijamii na kiuchumi kwao wenye ualbino, huku kukikosekana takwimu sahihi za watu wa kada hiyo kwa nchi nzima.

Pia, anaorodhesha changamoto nyinginezo ni: Umasikini; ajira kwao; mazingira magumu ya kupata elimu jumuishi; kukosekana bajeti jumuishi ya utoaji huduma za afya; na miongozo inayokinzana kuhusu utoaji matibabu ya saratani ya ngozi.

Mhazini Mkuu wa TAS Taifa, Abdillah Omar, analalamikia tozo wanayokumbana nazo kwenye mafuta yanayoingizwa nchini, kuwasaidia kujikinga dhidi ya mionzi ya jua.

Ombi lake kwa niaba ya chama, ni kwamba serikali ibadili msimamo katika tafsiri ya kiufundi kuhusu mafuta hayo, badala ya kuyaita 'vipodozi' iangaliwe ni 'dawa muhimu' kwani tafsiri iliyopo inaifanya kutozwa kodi kubwa inayofanya baadhi yao washindwe kuzimudu beo ya sasa, ilhali ni dawa ta ngozi yao.

"Mafuta haya ambayo yanatusaidia sisi ili ngozi zetu zisiweze kuharibika, yamekuwa yakichukuliwa kama anasa kwetu au aina ya vipodozi. Hivyo, hata yanapokuja kwenye makontena yanakuwa yameandikwa vipodozi, hali inayofanya kulipishwa kodi kubwa, tofauti na ilivyo kwenye dawa," analalamika.

Mhazini huyo wa TAS, anaendelea: "Maelekezo ya mafuta hayo mwenye ualbino yeyote atakayeyatumia, anatakiwa akae kwenye eneo ambalo halina jua, ila kutokana na ugumu wa maisha na kutafuta riziki wengine (wenye ualbino) hupaka na kisha kuingia mtaani."

### MAANDALIZI & MAFANIKIO

Katibu wa chama, Kabimba anaeleza kutokana na taifa kukabiliwa na ugonjwa corona, Sherehe ya Maadhimisho ya Miaka 40 zimepangwa kufanyika mwezi ujao kwa njia ya mtandao, ikishirikisha vyombo mbalimbali vya habari.

Anataja sehemu ya maudhui yake itajumuisha makongamano mtandaoni, redioni na vipindi vya luninga na redioni. Kabimba anaendelea:

"Chama kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine, tumefanikiwa kuwa na siku ya kitaifa ya kuongeza uelewa kuhusu ualbino ifikapo Juni 13 na tumeanza kuiadhimisha tangu mwaka 2006

"Chama chetu kilianzishwa mwaka 1978 na kusajiliwa rasmi mwaka 1980, ambayo kilikuwa na lengo la kuwaunganisha watu wenye ualbino na kutetea haki na maslahi yao ya kielimu, afya na ustawi wao ili kuondokana na dhana potofu kuhusu ualbino kwenye mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania," anasema Kabimba.

Kwa mujibu wa katibu huyo, tangu TAS isajiliwe Aprili 9 mwaka 1980, imefanikiwa kufikia mikoa 24 ya Tanzania Bara na zaidi ya wilaya 100, imekuwa ikishirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Watu Wenye Ualbino Zanzibar (JMZ), Anasema, ni hatua inayoifanya nchi kupiga hatua ya mbali na athari za wenye ualbino duniani, zilizopo sasa, Kabimba akiwa na ufafanuzi zaidi: "Nchi yetu ni miongoni mwa nchi chache duniani ambako sensa za watu na makazi, zinajumuisha watu wenye ualbino kwenye takwimu.

"Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 iliyofanywa na serikali kupitia Ofisi ya Takwimu, inaonyesha Tanzania ina jumla ya watu wenye ualbino16,376 ambayo TAS tumeweza kuwafikia 13, 364 (asilimia 81.60) kati yao 6,513 (48.7%) wakiwa ni wanaume na 6,851 (51.3%) wakiwa ni wanawake.

"Katika Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Miaka 40 ya kuanzishwa kwa Chama Cha Watu Wenye Ualbino, tutakwenda sambamba na maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa kuhusu Ualbino," anafafanua Katibu.

### MDAU MWANAMAMA

Mhamasishaji wa kinamama wenye ualbino, Christine Silas, anasema kinamama wenye ualbino wanakumbana na unyanyapaa, pindi wanapokuwa kwenye ujuzito, hata baadhi wakiwashangaa katika lugha anayonukuu "kumbe na huyu naye anaweza kubeba mimba? Nani kampa."

Christine anasema, hilo hujitokeza hata katika hatua ya kujifungua, wanakosa ushirikiano stahiki na tabia ya kuwashangaa kwa kejeli ikiendelezwa

"Tunaona vitu vingi vinakuwa vikitokea katika hospitali za serikali tofauti na hospitali za binafsi. Hivyo, tunaiomba serikali kulivalia njuga suala la unyanyapaa kwa watu wenye ualbino na kutoa elimu ya kutosha kwa wauguzi na wakunga," anasema.

Mama huyo anaendelea, chama chao kimeazimia kuandaa mdahalo wa afya ya uzazi na hedhi salama, ikilenga kuwapa elimu wauguzi na wakunga, kwani ndiyo kitovu cha kumpokea mtoto anayezaliwa, hasa akiwa na mama mwenye ualbino.

Katibu Mkuu wa TAS, Kabimba, anaweka majumuisho ya rai yao wote wenye mapenzi mema na wenye ulabino waweze kupata mahitaji muhimu kama mafuta ya kinga, miwani ya kukinga mionzi ya jua, vipeperushi na vijitabu mahitaji mengine ya kuibaili adha ya ugonjwa wa sasa corona.

"Yeyote mwenye mapenzi mema anaweza kuchangia maadhimisho haya kwa kupitia akaunti ya chama iliyopo Benki ya NMB Namba 20110003046," anasema Kabimba.

AFYA

MAADHIMISHO MIAKA 40

# Kisa saratani; umaskini unaua wenye ualbino wengi ujanani

Na Beatrice Philemon

JAMII ya watu wenye ualbino nchini, wanalalamika wengi kati yao wanafariki katika umri mdogo, kutokana na maradhi ya saratani ya ngozi.

Katibu Mkuu, Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Mussa Kabimba, anasema asilimia 75 yao wamezaliwa kwenye familia za wakulima na wafugaji, ambao kwa muda mrefu wanafanya kazi juani, hata wakaangukia katika kuugua saratani ya ngozi.

Anasema inatokana na kukosa rangi ya asili ya ngozi yenye uwezo wa kuhimili mionzi mikali ya jua na wakati huo huo, familia zao bado zina uelewa mdogo kuhusu uhalisi wa ualbino, matunzo yao na namna ya kuchukua tahadhari za kuwalinda kiafya.

Pia, Kabimba anasema watu hao wanafariki na saratani ya ngozi kwa sababu ya kukosa huduma za afya karibu na wanakoishi, pia rasilimali husika.

Ni kutokana na hilo, Kabimba anaiomba serikali kila inapopanga bajeti yake, iwafikirie kwenye suala la mafuta kinga na dawa nyinginezo waweze kufanya kazi zao vizuri.

"Kama wizara (Afya) itaingiza dawa muhimu kwa ajili ya ugonjwa wa kifua kikuu, saratani ya shingo ya kizazi, HIV (Ukimwi) na magonjwa mengine, basi na sisi watuagizie mafuta kinga ili kuimarisha afya zetu," anasema.

Anadokeza bei ya mafuta kinga yanayowasaidia wenye ualbino ni kati ya Sh. 35,000 hadi Sh. 75,000, ambazo ni zaidi ya uwezo wa jamii ya wenye ulabino.

"Inakadiriwa kuwa asilimia 75 ya watu wenye ualbino hawafikii umri utu uzima, kutokana na kufa mapema. Wengi wanapoteza maisha katika umri mdogo kuanzia miaka 32, 38 na 40 kutokana na saratani ya ngozi.

"Hii ni kutokana na taarifa tunazozipata kutoka kwa wazazi wao au walezi wao wanaowaleta kwa ajili ya matibabu katika hospitali (Taasisi ya Saratani) ya Ocean Road au hospitali nyingine," anasema

Kabimba anataja mwaka wa fedha uliopita, una jumla ya watu 18 wenye ualbino walifariki kutokana na saratani ya ngozi.

### HATUA KUJIHAMI

Anaeleza athari za kukosa vifaa tiba ni kama vile kukosekana mafuta kinga katika baadhi ya mikoa, baadhi yao wameamua kwenda kwa waganga wa kienyeji ambako wanabebeshwa sababu kwamba wamerogwa, hali inayochangia athari zaidi za saratani ya ngozi.

"Wengi hawana uwezo wa kulipa gharama za usafiri kutoka sehemu wanazoishi kuja katika Hospitali ya Ocean Road, Kilimanjaro Christian Medical Centre na Mwanza (Bugando) kupata tiba ya saratani ya ngozi," anafafanua.

Anawashauri wenye ualbino kucheki afya zao za ngozi kila mara, ili kama atagundulika ana tatizo apate matibabu ya awali mapema ya saratani ya ngozi, kabla ya kufika 'hatua ya tatu na nne' ambayo siyo nzuri na hatari sana.

Pia, anashauri waendelee kuvaa mavazi yanayofunika miili yao ili kukinga mionzi mikali ya jua na kama yakipatikana mafuta kinga(sunscreen lotions) kwa ajili ya kuboresha afya ya ngozi na kuzuia mionzi mikali ya jua, waendelee kutumia yanapopatikana.

Kabimba anasema, wakati Tanzania inajielekeza kwenye Sera ya Viwanda, anashauri serikali kuwahamasisha wawekezaji wa kigeni nchini, wakumbuke pia ujenzi wa viwanda vya kuzalisha mafuta kinga kwa ajili ya watu wenye ualbino nchini, kuwezesha kupatikana kwake kwa bei rahisi.

Anasema, wakati wanapoanzisha viwanda nchini, itasaidia kununua bidhaa hiyo kwa bei nafuu, pia watu wenye ualbino watakuwa na uhakika wa kupata huduma yenyewe.

Mbali na hilo, anatamka itawezesha Tanzania kuwa muuzaji wa mafuta hayo katika nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika na majirani wengineo.

"Mara nyingi tumekuwa tukikutana na wenzetu kutoka katika maeneo hayo kwenye mikutano mbalimbali, nao wanasema wana shida sana ya mafuta kinga katika nchi zao, kwa sababu hakuna viwanda vya kuzalisha bidhaa hii," anaeleza Kabimba.

Pia, anataja kuanzishwa viwanda vya kuzalisha bidhaa hiyo itakuwa fursa ya nchi kuuza katika nchi hizo, kwa sababu nako hakuna kiwanda chochote kinachozalisha bidhaa hiyo, wengi wanaagiza kutoka nchi za nje.

"Mafutakinga mengi yanayopatikana hapa nchini yanatoka katika nchi ya Uingereza, Canada, Sweden na Uholanzi ni ghali sana yanuzwa kati ya Sh. 35,000 hadi 75,000," anasema.

Pia, Chama cha TAS kinaomba watunga sera na wafanya uamuzi kutengeneza sera na miongozo maalum kwa ajili ya wenye ualibino, kama ilivyo kwa magonjwa kwa saratani za kizazi, titi na kifua kikuu, akiitaka serikali iongeze wataalamu wa matibabu ya ngozi na mahsusi wenye ualbino.

Vilevile anaomba watoto wenye ualbino wapelekwe shule, ili waweze kumudu mustakabali wa maisha yao, ikiwamo kumudu mahitaji ya hali zao kiafya.

Anasema Chama cha TAS kwa kushirikiana na serikali na wadau wa maendeleo, wamefanikiwa kuanzisha matibabu ya saratani ya ngozi kwenye hospitali za rufani katika mikoa saba, ikiwemo Lindi, Iringa, Tanga, Morogoro, Singida, Mara na Unguja.

Kwa mujibu wa Katibu huyo, lengo ni kusogeza huduma za afya kwa wenye ualbino na kupunguza vifo vinavyotokana na saratani ya ngozi kwao.

Kabimba anafafanua: "Mpaka sasa wameishasambaza vifaa tiba katika mikoa saba kwa ajili ya upatikanaji tiba ya awali ya saratani ya ngozi."

Anataja baadhi ya vifaa hivyo kwa majina: Brymil Dermatology; Cryogen; Liquid Nitrogen Container; Cryoplates; na Withdrawing Tube vilivyotumika katika upatikanaji tiba ya awali ya saratani.



Mussa Kabimba, Katibu Mkuu wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), akiwa na viongozi wenzake walipokabidhi vifaa tiba kwa madaktari wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro, kwa ajili ya kutibu saratani ya ngozi. **PICHA ZOTE: HISSANI YA TAS**

> **Mafutakinga mengi yanayopatikana hapa nchini yanatoka katika nchi ya Uingereza, Canada, Sweden na Uholanzi ni ghali sana yanuzwa kati ya Sh. 35,000 hadi 75,000.**



Katibu Mkuu, Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS), Mussa Kabimba, akimuonyesha Daktari wa Hospitali ya Rufani Mkoa Mara, kifaa tiba kinachotibu saratani ya ngozi kwa wenye ualbino.

AFYA

# Waziri Ummy: Ndivyo ilivyo shida iliyosumbua upimaji Covid – 19

• Aja na mbadala mpya aliyoubeba mkononi

**Na Yasmine Protace**

SERIKALI imetoa ripoti ya uchunguzi wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko jijini Dar es Salaam na kubaini upungufu mbalimbali wa kiutendaji.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anataja yaliyoainishwa na kamati hiyo, kwamba kuna mashine za kupima sampuli za Covid-19 zilikuwa na hitilafu na uongozi wa maabara na hakuchukuliwa hatua za kuifanyia matengenezo.

Taarifa hiyo pia imebainisha kuwapo upungufu katika mfumo wa kimuundo, kiutendaji na uendeshaji wa kitaaluma katika upimaji vipimo, uhakiki wa ubora wa majibu na udhaifu katika hifadhi ya vipimo vya Covid -19.

Waziri Ummy anatambulisha kuwapo upungufu wa wataalamu wenye sifa za mafunzo ya kitalamu yanayotiwa "Biotechnology & molecular Biology" katika sekta ya afya, hapo inajumuisha Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii.

Kutokana na majibu ya Kamati ya Uchunguzi wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii kuhusu upimaji wa sampuli za ugonjwa wa corona, Wizara ya Afya, Meandeleo, Jinsia, Wazee na Watoto, imechukua hatua kadhaa.

Ummy anazitaja kuwa ni kuhamisha shughuli za upimaji kutoka kwenye maabara iliyoko katika ofisi ya Taasisi ua Uchunguzi wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na kuanza kutumika mashine nyingine za maabara mpya iliyoko Mabibo, jijini Dar es Salaam.

"Kuanzia sasa shughuli zote za upimaji Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii zitafanyika katika maabara mpya ya Mabibo yenye vifaa vya kisasa, yenye ubora na uwezo wa kupima sampuli 1,800 ndani ya saa 24," anasisitiza Waziri Ummy.

Anaeleza kuwa maabara iliyokuwa inatumika awali na kukutwa na mapungufu, ilikuwa na uwezo wa kupima sampuli 300 kwa saa 24 na ilianzishwa mwaka 1968.

"Hivi sasa upimaji wa sampuli zote za Covid -19 umehamishiwa kwenye maabara hii ya Mabibo, Dar es Salaam, ambayo kuanzia sasa ndiyo itakuwa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii.

"Maabara hii ambayo ujenzi wake umekamilika mwezi huu, ina miundombinu inayojitosheleza, mashine za kisasa zinazoweza kupima sampuli nyingi na kutoa majibu ya uhakika na kwa haraka" anasema Waziri Ummy.

Aidha, Wizara imeshaandaa wataalamu zaidi wenye sifa na vigezo kwa ajili ya maabara hiyo na imeanza kurekebisha mfumo wa utawala, utendaji na kitaaluma ndani ya Maabara ya Taifa.

Waziri Ummy, aliunda Kamati ya wataalam iliyoanza kazi rasmi tarehe 6, Mei, 2020 ya kuchunguza mwenendo wa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, ikiwa ni pamoja na kuangalia mfumo mzima wa ukusanyaji na upimaji wa sampuli za Covid – 19.



Meneja wa Kitengo cha Sayansi Jinai, Biolojia na Vinasaba, Hadija Mwema, akimpa maelezo Rais Dk. John Magufuli, alipotembelea Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dar es salaam, Agosti mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

> **Hivi sasa upimaji wa sampuli zote za Covid -19 umehamishiwa kwenye maabara hii ya Mabibo, Dar es Salaam, ambayo kuanzia sasa ndiyo itakuwa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii.**

Kamati hiyo iliundwa kutokana na dodoso zilizoguswa na Rais Dk. John Magufuli hivi karibuni, akikosoa usahihi katika upimaji na husasan kutoka mabaara vya vipimo vya Covid - 1.

### MGANGA MKUU

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, katika ufanikishaji uwepo wa mazingira salama, anawakumbusha viongozi wa maeneo yote ya ibada, wahakikishe kunakuwapo vifaa vya kunawa mikono, maji tiririka na sabuni au vitakasa mikono kwa ajili ya usafi wa waumini katika maeneo ya kuingilia.

Prof. Makubi anashauri kuwa, sehemu za kuabudia ni budi kuwa na nafasi ya kukaa kati ya muumini mmoja na mwingine, iwe umbali wa zaidi ya mita moja kwa wale wanaokaa au kusimama.

Mganga Mkuu anafafanua kuwa, waumini wanapoenda kushiriki au kutembelea maeneo ya ibada na sala, wanashauriwa watumie barakoa za vitambaa ambazo kwa sasa zipo kwa wingi na zinatengenezwa nchini na wazalioshaji wazawa.

Rai nyingine kutoka kwa kiongozi na mtalamu huyo wa afya kitaifa, ni kwamba wananchi waepuke mikusanyiko na hasa isiyo na sababu, huku viongozi wa mikusanyiko hiyo ya kiimani wawakumbushe waumini wao kuzigatia kanuni ma miongozo iliyopo kiafya inavyoelekezwa na wataalamu wa afya

Mganga Mkuu wa Serikali, amewakumbusha wamiliki wa vyombo vya usafiri wa umma, kuzingatia maagizo ya serikali ya kutosimamisha abiria kwenye mabasi, vilevile wahudumu wote wawe wamevaa barakoa za vitambaa.

"Sheria zifuatwe, abiria wasisimamishwe na madereva wahakikishe wanavaa barakoa," anasema Mganga Mkuu.

### HISTORIA YAKE

Kwa mujibu wa tovuti ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ni kwamba mamlaka hiyo ni maabara teule ya serikali katika masuala ya uchunguzi wa kisayansi wa maabara.

Ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya mwaka 2016, ambayo kimuundo menejimenti yake inaongozwa na Mkemia Mkuu wa Serikali, akisaidiwa na wakurugenzi wa idara zilizo chini yake.

Wengine kwa mujibu wa taarifa hiyo, kuna mameneja wa kanda mbalimbali nchini na wakuu wa vitengo, wote wakisimama kama timu moja katika utekelezaji wa sera na miongozo inayotolewa na Bodi Tendaji.

Historia yake inaanzia mwaka 1895 katika kipindi cha Ukoloni wa Mjerumani, ilipokuwa chini ya Wizara ya Afya, kama Kituo cha Utafiti wa Magonjwa ya Ukanda wa Kitropiki, zikiwamo malaria na kifua kikuu.

Mwaka 1986 Maabara ya Mkemia Mkuu, iligeuzwa kuwa idara chini ya Wizara ya Afya. Kabla ya hapo, ilikuwa iliripoti kwa Mkurugenzi wa Huduma za Hospitali katika Wizara ya Afya.

Mkemia Mkuu wa Kwanza alikuwa Mjerumani, Gustav Giemsa, mwenye historia ya kugundua vidudu vinavyosababisha malaria na vimelea vya kifua kikuu, kwenye damu.

Ofisi za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Makao Makuu, zipo katika Barabara ya Barack Obama, jirani na Taasisi ya Utafiti wa Saratani Ocean Road, Dar es Salaam.

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pia inasimamia utekelezaji wa sheria tatu, ambazo ni: Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali Nchini; Vinasaba vya Binadamu (HDNA); na Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ya mwaka 2016.

***Makala inatokana na taarifa rasmi za afya serikalini na Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali.***



# Wakulima mtama waonyeshwa fursa

**Na Ibrahim Joseph, KONDOA**

WAKULIMA wa mtama mweupe nchini, wametakiwa kuchangamkia fursa ya soko la uhakika kutokana na kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kuhitaji kwa wingi kwa ajili ya uzalishaji wa vinywaji vyake.

Hayo yalibainishwa na Meneja Kilimo wa TBL, Joel Msechu, wakati alipokuwa akizungumza juzi na wananchi wilayani hapa kwa nyakati tofauti kuhusu kilimo hicho na uhitaji wa zao hilo.

Msechu alisema kampuni hiyo inawahakikishia soko la uhakika wakulima wa mtama kuwa linahitajika kwa ajili ya viwanda vya kampuni hiyo kuzalishia vinywaji, hivyo wakulima wachangamkie fursa hiyo.

Alibainisha kuwa lengo la ziara ya wataalamu wa kilimo wa kampuni hiyo kuwatembelea wakulima katika maeneo hayo ni kukagua aina ya mtama unaohitajika kwao.

Kadhalika, alisema lengo la kufika kuzungumza na wananchi ni kuwajulisha bei zinazotumika kununua zao hilo ili kuepuka kuingia mikononi mwa madalali.

Pia, alisema katika msimu wa mwaka huu kampuni hiyo inanunua zao kwa bei ya Sh. 550 kwa kilo moja kwa mtama huo unaohitajika na wataweka vituo kila maeneo watakayonunua zao hilo.

Aidha, Msechu alisema, kuna baadhi ya wakulima nchini wamewezeshwa mbegu bora za kilimo cha mtama katika msimu wa mwaka huu kwa lengo la viwanda vya kampuni hiyo kuzalisha aina ya bia inayotengenezwa hapa nchini.

Alisema katika idadi hiyo wakulima 1,398 wapo katika Wilaya ya Kongwa na wamewezeshwa mbegu hizo kwa lengo la kuvuna mazao bora.

Aliongeza kuwa TBL, inashirikiana na vituo vya Taasisi ya Utafiti wa Mazao (Tari) kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hao mbegu bora ya mtama, ambayo itatumiwa kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Baadhi ya mikoa waliyoanza nayo katika uzalishaji wa mbegu bora ni Dodoma, Singida, Manyara na mategemeo ni kuendelea na mikoa mingine katika msimu wa 2020/2021.

Msechu alisema kupitia utafiti huo wanategemea idadi ya wakulima wa mtama itaongezeka kwa sababu watakuwa na uhakika mbegu inayofaa katika maeneo yao na kutakuwa na soko la uhakika kwa mtama wote utakaozalishwa.

Alisema viwanda vyao vinahitaji mtama zaidi ya tani 15,000 kwenye viwanda vyao vinne vilivyopo nchini, hivyo wakulima wachangamkie kilimo hicho ili kuinua uchumi wao.

Mkulima Issa Dinya, wa kijiji cha Bumbuta, aliishukuru TBL kwa kuwahakikishia soko la zao hilo ambalo awali lilikuwa limeshaanza kuwakatisha tamaa ya kuendelea kulilima.

# Waziri Jafo atahadharisha uwekezaji feki elimu Kibaha

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameutahadharisha uongozi wa Shirika la Elimu Kibaha kuwa makini na uwekezaji utakaofanyika ili uwe na tija.

Jafo alitoa tahadhari hiyo jana jijini hapa wakati wa kuzindua Bodi mpya ya Shirika hilo inayoongozwa na Prof. Raphael Chibunda.

Alisisitiza kuwa uwekezaji wowote watakaoamua kuufanya lazima uwe na uwekezaji wenye tija ili kuepuka watu wajanja watakaoenda na maandiko feki na kufanya uwekezaji usiokuwa na tija.

"Shirika la Elimu Kibaha lina ardhi kubwa sana, ambayo kama mtakuwa wabunifu mtakuja na uwekezaji ambao utasaidia sana kuimarisha uchumi wa shirika, mnaweza kuja na maduka ya kisasa pale," alisema.

"Shirika limekuwa na rasilimali nyingi ikiwamo ukubwa wa ardhi ambao kama bodi itafanya ubunifu itaweza kuitumia kufanya uwekezaji wenye tija utakaosaidia shirika kujiimarisha kiuchumi na kujitegemea," alisema.

Kadhalika, Jafo alisema ni vyema bodi hiyo ikaendeleza na kuchagiza maono ya Baba wa Taifa, Julius Nyerere ambaye aliamua kuanzisha shirika hilo ili kupambana na maadui watatu ujinga, maradhi na umaskini.

"Niipongeze Hospitali ya Tumbi kwa kuja na ubunifu wa kutengeneza maji tiba (drip), ambao umesaidia kuipunguzia serikali gharama za kuagiza maji hayo sambamba na Shule ya Sekondari Kibaha na Chuo cha Ufundi (TDF), kufanya vizuri," ilisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Chibunda, alisema bodi yake inakwenda kutekeleza maagizo aliyoyatoa na kulifanya shirika liimarike zaidi.



Kinamama wauza mboga, wakipanga mchicha wao chini bila ya kuufunika eneo ambalo ni rahisi kuingia vumbi kutokana na magari na waenda kwa miguu kupita, nje ya soko kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya za walaji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Tamwa yaonya matumizi mabaya mitandao

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WATUMIAJI wa mitandao wametakiwa kuwa makini katika matumizi ya teknolojia hiyo kwa kuweka taarifa ambazo hazitakuwa na madhara kwao ili kuepuka mkono wa sheria.

Akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari wa jijini hapa Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Rose Reuben, alisema kuna baadhi a watu wamekuwa wakiweka vitu mbalimbali zikiwamo picha ambazo baadaye zinadhalilisha utu wao.

Alisema Tamwa inatoa mafunzo hayo kwa wanahabari kwa kuwa ni kundi muhimu linalotumia zaidi teknolojia ya mtandao ili wapate uelewa wa kutosha wa kutumia mitandao.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa wanahabari ili wapate uelewa mpana wa matumizi ya teknolojia hii, lakini waweze kujilinda kimtandao," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema lazima mwandishi ajue athari za kutumia mitandao na ajue maisha yake kimtandao yakoje badala ya kutuma vitu zikiwamo taarifa binafsi mitandaoni bila kujua athari zake.

"Tunatakiwa kubadilisha fikra katika kuishi kimtandao, lazima tujue kwamba historia ya mtandaoni haifi miaka na miaka na kimsingi zinaleta athari," alisema.

Pia alisema mafunzo hayo ni muhimu kwani kutokana na kubadilika kwa mitindo ya maisha na jinsi teknolojia inavyokua, upo uwezekano mkubwa mambo mengi kufanyika kimtandao katika miaka ijayo.

"Tumeona kipindi hiki cha corona, vitu vingi vinafanyika mtandaoni ikiwamo mikutano...tumeanza hivyo, lakini miaka ijayo hali hiyo inaweza kuendelea," alisema Reuben.

Ofisa Mradi wa Usalama mtandaoni unaoendeshwa na Tamwa, Godwin Assenga, alisema ili kuepuka matumizi mabaya ya kimtandao, sharti watumiaji wa mitandao wawe na mazoea ya kuhifadhi taarifa zao kwa usiri wa hali ya juu.

"Usiri unahitajika tunapoweka vitu mtandaoni, tuepuke kuweka vitu vyetu wazi hali hii inasababisha watu kutujua zaidi na kupata shauku ya kutuharibia maisha yetu kupitia mitandao," alisema Assenga.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema wamejifunza mambo mengi huku wakisema kuna baadhi ya mambo walikuwa wakiyafanya mitandaoni ikiwamo kutuma picha na kuweka baadhi ya mambo ya kifamilia, wakidhani walikuwa sahihi kumbe walihatarisha usalama wao mitandaoni.



# Wanane washikiliwa tuhuma za kujeruhi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watuhumiwa wanane kwa tuhuma za kushiriki tukio la kujeruhi baada ya kutokea ugomvi kati ya raia wa China wanaomiliki kampuni ya michezo ya kubahatisha (Bonanza) na watu waliokuwa wanacheza mchezo huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani humo, Ulrich Matei, Mei 25, 2020 majira ya saa 12 jioni maeneo ya Soweto, Kata ya Ruanda, jijini Mbeya, watu wawili ambao ni Abison Hamis (36) na Gilbert Mwakanyemba (32), mjasiriamali wote wa kazi wa Manga Veta, walijeruhiwa kwa kukatwa panga sehemu mbalimbali za miili yao na raia wa China kwa kushirikiana na baadhi ya wafanyakazi wao.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni ugomvi uliozuka kati ya ChenYen (43) mfanyabiashara, raia wa China, mkazi wa Veta na Hamis baada ya kutamka neno la Kichina lililomuudhi Yen na kusababisha ugomvi uliosababisha baadhi ya watu kujeruhiwa.

Kufuatia tukio hilo, raia huyo wa China alipiga simu kuomba msaada kwa wenzake ambao ni raia wa China ndipo walifika na kuanza kuwashambulia Hamis na Mwakangemba kwa panga maeneo mbalimbali ya miili yao, hali iliyosababisha kupata majereha makubwa na kukimbizwa katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya kupata matibabu.

Kutokana na tukio hilo, alisema msako mkali umefanyika na watu wanane wamekamatwa ambao ni Chen Yen, Xiao Jing, Lin Hai, Lyu Qzing, Jiang ze Dong, Gift Elia Herman Elias Kenedy Mwamlima na kwamba upelelezi unaendelea.

Katika hatua nyingine jeshi hilo limefanikiwa kumkamata Richard Boniface (31), mkazi wa Kata ya Matundasi wilayani Chunya akiwa na gramu 245 za bangi, na kwamba mtuhumiwa huo ni muuzaji na mtumiaji.

**Kufuatia tukio hilo, raia huyo wa China alipiga simu kuomba msaada kwa wenzake ambao ni raia wa China ndipo walifika na kuanza kuwashambulia Hamis na Mwakangemba kwa panga maeneo mbalimbali ya miili yao, hali iliyosababisha kupata majereha makubwa na kukimbizwa katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya kupata matibabu.**

# Barabara tano kujengwa kwa lami

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi na Mawasiliano, imepitisha barabara tano kwa ajili ya kujengwa na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji.

Hayo yalisemwa juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, wakati akitoa taarifa kwa Baraza la Madiwani juu ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye halmashauri hiyo.

Mwalingo alisema serikali ilipitisha barabara tano za ndani na zinazopita katika halmashauri yao ili zijengwe kwa kiwango cha lami ikiwamo ya Mbalizi-Mkwajuni, Itewe na Inyala kuharakisha shughuli za kimaendeleo pamoja na zile ambazo zinatarajiwa kujengwa na Wakala wa Barabara za mijini na vijijini Tarura pamoja na Ujenzi wa Kituo cha mabasi Tarafani kilichopo mjini Mbalizi.

"Kukamilika kwa barabara hizi ambazo zinagharimu zaidi ya bilioni nne, kutasaidia kuongeza mapato ya halmashauri, kutarahisisha shughuli za usafirishaji mazao kama vile mahindi, viazi, maharage, njegere na pareto muhimu ni kuwahimiza wataalamu wa wilaya na Tanroads kukamilisha barabara hizo kwa wakati," alisema Kisemba.

Sambamba na hayo, Kisemba aliliambia Baraza kuwa Wilaya ya Mbeya imefanikiwa kupata umeme kupitia mradi wa Rea ambapo asilimia 90 ya vijiji vina umeme.

"Tunapoongea jitihada mbalimbali zinazofanywa na madiwani katika kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya kama vile Ilembo ambacho kimesaidia wananchi kuondokana na adha ya kutumia umbali mrefu kufuata huduma za afya," alisema Kisemba.

Vilevile, uondoshaji wa tozo kwa wajawazito waliokuwa wanachelewa kuanza kliniki au wengine kujifungulia njiani.



Viongozi wa dini ya Kikristo mkoani Mbeya, wakifanya maombi jana, maalumu katika eneo inapojengwa ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo, ili ujenzi huo usipate vikwazo ambapo pia waliwaombea viongozi mbalimbali wa kitaifa akiwamo Rais John Magufuli, ili aendelee kuwa jasiri katika kuliongoza taifa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Uwekezaji Ziwa Nyasa watajwa fursa kuongeza idadi ya watalii

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

UWEKEZAJI kwenye Fukwe za Ziwa Nyasa zilizopo wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya, unadaiwa kuwa unaweza kuongeza idadi ya watalii katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini na kuinua uchumi wa Taifa endapo kutakuwa na wawekezaji wa kutosha.


Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati akikagua miundombinu ya barabara kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa ambapo aliwakaribisha watu wenye uwezo kuwekeza kwenye fukwe za ziwa hilo.

Alisema Wilaya ya Kyela ina fukwe nzuri mwambao mwa Ziwa Nyasa na, kwamba hata kina cha ziwa sio kirefu sana, hii ni fursa sasa kwa wadau kutumia fursa ya kujenga hoteli na miundombinu mingine ambayo itavutia watu kutembelea.

"Bichi zote hizi za Kyela zikiboreshwa zitachochea maendeleo na hata kwa wavuvi itakuwa neema kwao kwani samaki walaji watakuwa karibu jambo la muhimu sasa ni kuboresha miundombinu ya barabara ili fukwe zote ziweze kufikika kirahisi," alisema Chalamila.

Aidha, Chalamila alisema uwapo wa meli mbili mpya za mizigo na moja ya abiria ambazo zimejengwa na Serikali ya Tanzania ndani ya Ziwa Nyasa pia ni kichocheo kingine cha biashara inayoweza kuinua uchumi kwa Watanzania kupitia Ziwa Nyasa.

Aliongeza kuwa katika kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji katika mwambao wa Ziwa Nyasa lenye fukwe nzuri za mchanga ambazo zinafanana ishwa na fukwe za visiwa vya Unguja na Pemba, tayari serikali ya Tanzania imekamilisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 39.1 kwa kiwango cha lami kuanzia eneo la Kikusya hadi Matema ambayo inarahisisha usafiri wa kuzifikia fukwe nzuri za Ziwa Nyasa.





## Wanaume 43 walipa matunzo familia kupitia serikali

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

JUMLA ya wanaume 43 wamesajiliwa na kuanza kupeleka fedha za matunzo ya watoto serikalini kutokana na kushindwa kutunza familia vizuri baada ya wazazi wawili kutengana.

Naibu Waziri wa Uwezeshaji Wanawake, Wazee na Watoto, Shadya Suleiman, aliliambia Baraza la Wawakilishi kwamba wizara ipo makini kuona wanaume wanaotelekeza familia zao ikiwamo watoto baada ya kutengana wanabanwa na kuzitunza familia hizo.

Alisema migogoro mingi ya wanaume kushindwa kutunza familia inatokana na familia kutengana na tatizo la talaka holela zinazotolewa bila ya kuzingatia maadili ya ndoa.

"Wizara ya Wanawake, Watoto na Wazee, tumefanikiwa kuwabana wanaume wanaoshindwa kutunza familia zao kuhakikisha wanawasilisha fedha za matunzo wizarani," alisema.

Hata hivyo, alisema wanashindwa kuwabana wanaume wengine wanaotelekeza familia zao ambao ni watumishi wa serikali kutokana na kipato kidogo cha mshahara wao, huku wengine wakikabiliwa na mikopo mingi.

"Wapo wafanyakazi wengine tumeshindwa kuwabana na kuwakata mishahara yao kwa ajili ya kuhudumia familia zao walizozitelekeza kwa sababu mishahara yao ni midogo, huwezi kuigawa sehemu mbili na wengine wakikabiliwa na mikopo," alisema.

Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio, mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2020-2021, walisikitishwa na tatizo la wanaume kutelekeza familia na utoaji wa talaka kiholela unaosababisha watoto kutelekezwa.

**"Wizara ya Wanawake, Watoto na Wazee, tumefanikiwa kuwabana wanaume wanaoshindwa kutunza familia zao kuhakikisha wanawasilisha fedha za matunzo wizarani," alisema.**

# Vyuo vikuu, kidato cha sita kuanza masomo Juni mosi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imetangaza kuruhusu wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja na kidato cha sita kuendelea na masomo yao ifikapo Juni mosi baada ya vyuo hivyo kufungiwa kutokana na ugonjwa wa corona.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alisema hayo wakati akitoa taarifa rasmi ya serikali kuhusu kulegeza masharti ya kupambana na corona.

Alisema wanafunzi wa vyuo vikuu na kidato cha sita wataendelea na masomo yao kwa sababu wanakabiliwa na jukumu la mitihani ya mwisho wa mwaka.

Alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imetakiwa kukaa pamoja na Wizara ya Afya kuweka mwongozo utakaoruhusu kuanza kwa masomo hayo ikiwamo tahadhari za kupambana na ugonjwa huo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua uamuzi wa kulegeza masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa Covid-19 na sasa tunaruhusu wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja na kidato cha sita kuendelea na masomo yao kwa ajili ya matayarisho ya mitihani ya taifa," alisema.

Balozi Iddi alisema serikali imechukua uamuzi huo wa kulegeza masharti ya kuruhusu wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja na kidato cha sita kuendelea na masomo yao baada ya kuwapo kwa mafanikio makubwa katika kupambana na ugonjwa huo ikiwamo maambukizo.

Alisema shughuli za michezo ikiwamo Ligi Kuu ya Zanzibar ambayo ilisimama kutokana na kuwapo kwa ugonjwa huo, sasa itaendelea Juni 5, viongozi wa Wizara ya Vijana, Utamaduni na Sanaa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Shirikisho la Soka la Zanzibar (ZFF), watakaa pamoja kuweka mwongozo na kanuni za kuendesha ligi hiyo.

Balozi Iddi alisema, upande wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ikiwamo kidato cha nne hadi cha tano, shule zao zitaendelea kufungwa hadi watakapopata maelekezo mengine.

Kadhalika alisema, hali ya mwenendo wa ugonjwa wa Covid-19 kwa upande wa Zanzibar imedhibitiwa kwa kuwa na wagonjwa 19 waliolazwa katika vituo vya kupata huduma vilivyopo Unguja na Pemba.

Alisema wagonjwa watatu wamelazwa katika kituo cha afya kilichopo vitongoji Pemba na hali zao ni nzuri huku wagonjwa 19 wakilazwa vituo vya Unguja.

"Napenda kuwajulisha wananchi kwamba kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa Covid-19 kwa kupunguza wagonjwa kutoka 134 hadi kufikia 19 ambao wanaendelea na matibabu na hali zao ni nzuri," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujilinda na ugonjwa huo ambao bado ni tishio kwa afya za wananchi.

Pia, aliwataka wananchi kuondoa hofu na kufanya kazi zao za kujipatia riziki pamoja na ujenzi wa taifa huku wakichukua tahadhari za ziada.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kusini Unguja, Rashida Rashid Abdallah, akikagua gari ya abiria katika eneo la Tunguu, mkoani humo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ujenzi vyuo vya amali wafikia pazuri

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali unaoendelea vizuri na umefikia hatua ya kukamilika kwa ajili ya kupokea wanafunzi kupata elimu ya ujasiriamali ya kuwawezesha kujiajiri.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu hoja za wajumbe waliochangia bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Pemba alisema ujenzi wa vyuo hivyo ni mkombozi kwa vijana katika kujiajiri na kuacha kutegemea ajira serikalini ambazo ni chache.

Alivitaja vyuo vitakavyojengwa chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfD) kuwa ni Makunduchi pamoja na Daya Mtambwe, Pemba.

Alisema Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Makunduchi, ujenzi wake umefikia asilimia 79, huku ujenzi wa Daya Mtamwe umefikia asilimia 87.

"Mheshimiwa Spika napenda kutoa habari nzuri kuhusu maendeleo ya ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali kwa upande wa Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, umefikia asilimia 79, wakati Chuo cha Mafunzo kilichopo Daya Mtambwe, umefikia asilimia 87," alisema.

Alieleza kuwa, ujenzi wa vyuo hivyo ni sehemu ya mikakati ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kuona vijana wanajiajiri katika sekta binafsi na kuacha kutegemea ajira serikalini.

Alisema baada ya kukamilika kwa vyuo hivyo na kuanza kupokea wanafunzi mbalimbali, matarajio ya serikali ni kuona vijana wanapata ujuzi wa kazi za mikono na ufundi.

"Hayo ndiyo malengo ya kuanzishwa kwa vyuo vya mafunzo ya amali na ufundi nchini kuona vijana wanajiajiri katika sekta binafsi na kupata kazi za ujuzi za ufundi na kuacha mawazo ya kutegemea ajira serikalini," alisema.

Alizitaja sababu zinazosababisha vyuo hivyo kuchelewa ujenzi ikiwamo kuwapo kwa tatizo la uhaba wa rasilimali ya mchanga.

"Nchi yetu kwa sasa inakabiliwa na tatizo la uhaba wa mchanga...ilifika wakati wizara ilisitisha upatikanaji wa mchanga kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa rasilimali hiyo," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE LAND ACT, 1999**
**(NO. 4 OF 1999)**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**
**Date: 27/05/2020**
**Ref No: KUTC/LD/67020/HKK**
**APPLICANT: JOCTAN MAGANGA NGELLY**
**REGISTERED OWNER: JAMES LUKONA**
**LAND;**
**PLOT NO: 26 BLOCK: "M" HD: LOCATION: VAMIA MWANGA**

Take notice that, the Original Letter of Offer of the land described above is said to be lost and I intend to issue a Certified True Copy of the original Letter of Offer in lieu thereof unless causes to the contrary is shown within one month from the date of this publication.

The original Letter of Offer if found, should be delivered to the Office of Municipal Director of P.O. Box 44 Kigoma.

157537

## KUPOTEA KWA PASIPOTI/ HATI YA KUSAFIRIA



**De'Ichance Mwajuma Nuru** anatangaza kupotea kwa Passport/hati ya kusafiria yenye namba AB798938 iliyotolewa na Ofisi za Uhamiaji mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2016, Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochotec cha Polisi.
**Polisi Taarifa:**
**PWA/KIB/RB/359575/2020**

157525

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ABUBAKARI HAMIS MOHAMED anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 910 BQF.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi:
KRT/RB/578/2020.

157529

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

JAMES MURIMI NDULLA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 838 DET (REGIUS ACE – TOYOTA). Chassis namba TRH1125006959. Engine namba 1TR0036738. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/MAG/RB/378496/2020.**

157527

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEVEL KISHORE SOLANKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 500 BJZ MARK II GX110. Chassis namba GX1106010713. Engine namba 1GFE6833219. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DSM/PHQ/RB/401234/2020.**

157528

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID ULF NILSON anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 881 CLQ (RAV 4). Chassis namba ZCA260042940. Engine namba 1ZZ1445976. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/MAG/RB/578476/2020.**

157526

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA.

Bwana **TITUS WILLIAM LUHENDE** anatangaza kupotelewa na ofa ya kiwanja yenye Namba 46 Kitalu "K" (HD), Central Area Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakayeiona anaombwa kutoa taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.

Taarifa:
**ARU/ARU/RB/401627/2020.**

157524

**TANGAZO**
**Katika Mahakama ya Mwanzo…… Moshi Mjini……………………………………………………**
**Usimamizi wa Mirathi No, …..63………..2020**

**Ombi la MENYIAICHI ANASEL MALIMO NA THOMAS JUSTINE SHOO**

**Usimamizi wa mirathi ya marehemu JUSTINE ANASEL SHOO**

Kwa …..Yeyote anaehusika Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa
Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo ….11…/06/….2020………kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa .

Tarehe ….26….05….2020…………………

157533

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**SHAURI NAMBA 1 LA 2020**
**SAID HASSAN……………………..MDAI**
**DHIDI YA**
**JANE ZEBEDAYO, BAKARI MOHAMED NGAGE, ABDALLAH M. NGAGE, RAMADHANI A. ABDALLAH KOMBO………………...WADAIWA**

KWA: BAKARI MOHAMED NGAGE, ABDALLAH M. NGAGE, RAMADHANI A. ABDALLAH KOMBO…POPOTE MLIPO.

SAID HASSAN amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 28/5/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na muhuri/Lakiri wa Baraza hii leo tarehe 15/5/2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TANGA

## KUPOTEA KWA CHETI



**FEBRONIA DEOGRATIUS KASONOKO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0989/0011 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIBARA SEKONDARI mwaka 2016.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: KBR/RB/464/2018.**

157503

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**DODOMA MJINI**

**<u>Usimamizi wa mirathiNA. 42/2020</u>**

Ombi la **AZIZI ALLY SHAMTE** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu
**ALLY AZIZI SHAMTE**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 25-06-2020 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 21/05/20

157512

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AMOUR UTALI BAKAKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI yenye namba za usajili T 438 BKV.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MAN/KIT/RB/395183/2020.**

157514

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARI IDD ALLY** anatangaza **kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 768 DDR TOYOTA LITEACE. Colour GREY METALIC OPAL. Chassis namba JT711SR4000043345. Engine namba 35152017.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya Polisi:**
**TAN/RB/400324/2020.**

157511

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ATHUMAN IDDY OMARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 156 DSB TOYOTA VITZ. Chassis namba NCP150060184. Engine namba 2NZ3352058. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi:
DAR/KUB/RB/399588/2020.

157501

## NYARAKA ZIMEPOTEA

**JUMA S. LOSSINI** anatangaza kupotelewa na nyaraka zake zifuatazo:
Vyeti vya Hisa za CRDB Bank PLC(CRDB A/C No. 185260,CDS A/C No 199841),
Kadi ya gari yenye namba ya usajili T972 AKJ-Toyota na cheti cha Hisa cha TCCIA.
**Atakayezipata azipeleke kituo cha polisi kilichopo karibu.**

**AR/RB/417/2019 au apige simu Na. 0736003839.**

157502

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Bavicha yadai kushangazwa tuhuma unyanyasaji kingono

**Na Enock Charles**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), limeeleza kushangazwa na tuhuma za unyanyasaji wa kingono zilizotolewa na wabunge wawili wa viti maalum waliohamia chama cha NCCR-Mageuzi hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa baraza hilo bara, Moza Ally, alisema malalamiko hayo yaliyotolewa Ijumaa iliyopita na wabunge hao katika vyombo vya habari hayajawahi kutolewa popote katika idara za chama hicho na kudai kuwa yamelenga kukichafua chama hicho.

"Ndiyo mara ya kwanza tumesikia watu wazima wenye watoto wakisema kuwa wamenyanyaswa kingono, mnapaswa kujiuliza hawa watu wamekaa bungeni kwa takribani miaka mitano sasa," alisema Moza.

"Hajawahi kusema huko nyuma waje kusema sasa tunapoelekea kwenye uchaguzi, kwetu sisi hiyo ni nia ovu ya kukichafua chama," alisema.

Suzanne Masele na Joyce Sokombi, kutoka katika chama hicho walitangaza kukihama chama pamoja na mambo mengine walitaja sababu iliyoafanya waondoke ni kukosekana kwa uwazi kwenye matumizi ya fedha.

Akifafanua michango hiyo, Mbunge Masele alisema wabunge wa viti maalum wamekuwa wakichangia chama hicho Sh. milioni 1.5 kila mwezi tangu Januari mwaka 2016 hadi Aprili 2019 kwa miezi 40 na kufanya jumla ya michango hiyo kufikia Sh. bilioni 2.2 ikiwa ni mchango wa Sh. milioni 62 kwa kila mbunge.

Alidai kuwa suala hilo ni kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho, lakini kinachokosekana ni uwazi kwenye matumizi yake na hawaruhusiwi kuhoji kokote.



Magari yakipita kwa tabu katika barabara ya kwenda Msanga Zalala, eneo la Chanika, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam jana, iliyoharibiwa na mvua zilizonyesha hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ufaransa yatoa mkopo wa bil. 175/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesaini mkataba wa mkopo na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) wenye thamani ya Sh. bilioni 175.6 kwa ajili ya kugharamia mradi wa Majisafi na Majitaka, mjini Morogoro.

Akizungumza jana katika hafla ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, alisema wakazi wa Mjini Morogoro 772,010 watapata majisafi kupitia mradi huo ambao utafanyiwa upanuzi wa mfumo wa usambazaji wa maji.

Alibainisha kuwa ukikamilika utaongeza majisafi kutoka mita za ujazo 37,000 kwa siku hadi kufikia mita za ujazo 108,000 kwa siku.

"Hii itachangia katika kufikia malengo ya mahitaji ya majisafi yanayokadiriwa kuwa mita za ujazo 126,253 kwa siku ifikapo mwaka 2035 kwa wakazi wa Morogoro,"alisema.

Alisema mradi huo utaongeza upatikanaji wa huduma za majitaka kutoka kiwango cha sasa cha asilimia tano hadi 15 kwa wakazi hao.

"Nchi zetu mbili zina uhusiano mzuri unaoendelea kukua unaothibitishwa kupitia idadi ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na AFD, ambayo inaendelea na ile inayotarajiwa kuanza hivi karibuni, Tanzania imekuwa ikinufaika na ufadhili wa AFD hususan katika sekta za Nishati, Maji na Usafirishaji na Kilimo," alisema.

Alitolea mfano miradi inayoendelea inayofadhiliwa na AFD kwa misaada na mikopo kufikia Sh. bilioni 387.6.

"Napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ajili ya miradi ambayo ipo katika maandalizi, ambapo AFD wameonyesha nia ya kutoa mikopo ya masharti nafuu na misaada ambayo inafikia Sh. trilioni 2.39.

Naye, Mkurugenzi wa Shirika hilo nchini, Stephanie Mouen Essombe, alisema lengo la mradi huo ni kuimarisha hali ya maisha, mazingira pamoja na maendeleo ya kiuchumi ya mji kupitia upanuzi na marekebisho ya miundombinu ya majisafi na majitaka.

"Kwa niaba ya Serikali ya Ufaransa ninawahakikishia kuwa tutaendelea kuisaidia Tanzania, mradi huu umekuja wakati muafaka wa mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 yakiendelea na tunajua maji ni nyenzo muhimu katika mapambano haya,"alisema.


ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

## BEI ZA UMEME KWA WAPANGAJI KWENYE MAJENGO YA MAKAZI NA BIASHARA

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 17 cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414, Kifungu Na. 23(1) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 na Kanuni Na. 17 ya Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za mwaka 2017, Tangazo la Serikali Na. 452 la mwaka 2017, AMRI inatolewa kwa wamiliki wa majengo ya makazi na biashara kwamba bei za umeme kwa ajili ya wapangaji wao isizidi bei zilizoidhinishwa na EWURA kama zinavyoonekana hapa chini na kama zitakavyorekebishwa na kuidhinishwa na EWURA mara kwa mara. Aidha, bei pekee za umeme zitakazotumika ni zile ambazo zitatangazwa na EWURA kupitia Gazeti la Serikali. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki yeyote atakayekiuka amri hii.

| Kundi la Mteja | Bei/ Tozo | Uniti | Bei Zilizoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| D1 | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | - |
| | Bei ya Nishati (0 - 75 kWh) | TZS/kWh | 100 |
| | Bei ya Nishati (Zaidi ya 75 kWh) | TZS/kWh | 350 |
| T1 | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | - |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 292 |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/Mwezi | - |
| T2 | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | 14,233 |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 195 |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/Mwezi | 15,004 |
| T3 - MV | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | 16,769 |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 157 |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/Mwezi | 13,200 |
| T3 - HV | Tozo ya kutoa Huduma | TZS/Mwezi | - |
| | Bei ya Nishati | TZS/kWh | 152 |
| | Bei ya Mahitaji ya Juu | TZS/kVA/Mwezi | 16,550 |

**Muongozo**

D1: Wateja wa majumbani ambao wana matumizi madogo ya wastani wa uniti 75 kwa mwezi. Matumizi yatakayokizidi uniti 75 yatatozwa bei ya juu ya Shilingi 350 kwa kila unit moja inayozidi. Kwa kundi hili la wateja, umeme unatolewa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V).

T1: Wateja wenye matumizi ya kawaida hususani wateja wa majumbani, kwenye biashara ndogondogo, viwanda vidogo, taa za barabarani, mabango n.k. Umeme unatolewa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V) na njia tatu (400V).

T2: Wateja wenye matumizi ya kawaida ya umeme kupitia 400V na matumizi kwa mwezi ni zaidi ya uniti 7,500.

T3-MV: Wateja walioounganishwa katika msongo wa kati wa umeme (Medium Voltage).


T3 - HV: Wateja walioounganishwa katika msongo mkubwa wa umeme (High Voltage) ikijumuisha ZECO, Bulyanhulu na Twiga Cement.

**Mhandisi Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

157538

## HABARI MICHEZO

# JUVE HAIWEZI KUMSAJILI TENA POGBA



**TURIN,** Italia

NYOTA wa Manchester United, Paul Pogba kurudi Juventus inaonekana kuwa ni jambo lisilowezekana kwa sasa, kwa mujibu wa gazeti la Corriere dello Sport.

Pogba mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Old Trafford, huku Juventus na Real Madrid zikitajwa kuwania saini ya kiungo huyo.

Lakini kwa upande wa miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, inaonekana kwamba dili hilo kwa sasa haliwezekani kwa upande wao.

Kwa mujibu wa ripoti za nchini Italia, Juventus sasa wamekata tamaa ya kumrudisha Pogba pale Turin, kwani matatizo ya kifedha yaliyoikumba klabu hiyo kutokana na milipuko ya virusi vya corona, ndio sababu za kuyumba kifedha.

Corriere dello Sport limebainisha kwamba Bianconeri hao hawana uwezo wa kulipa euro milioni 100 kwa United kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

"Ni jambo gumu kwa Juventus kwa sasa, uwezekano wa kulipa euro milioni 100 ambazo ndio gharama ya Pogba ni mdogo," liliandika gazeti la Corriere dello Sport.

Pogba aliondoka Juve kujiunga na United kwa ada ya euro milioni 105 mwaka 2016 ambayo iliweka rekodi.



# Kocha Bayern asifia kipaji cha Sancho

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick amesifia "kipaji kikubwa" cha Jadon Sancho, huku akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Borussia Dortmund.

Sancho alitokea benchi wakati Dortmund ikipokea kichapo cha bao 1-0 kwenye mchezo baina ya timu hizo juzi Jumanne kwenye mchezo wa ligi na hivyo sasa imeachwa mbali katika mbio za kuwania taji la Bundesliga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 20 amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo, huku Bayern Munich na klabu kadhaa za Ligi Kuu England zikihusishwa naye.

Flick aliulizwa kuhusu Sancho baada ya ushindi huo wa Bayern na alisifia sana uwezo wa mshambuliaji huyo.

"Sipendi kuzungumza wachezaji ambao wapo chini ya mikataba na klabu nyingine," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Naweza kusema kwamba, Jadon Sancho ana ubora wa juu, lakini anafanya vizuri sana pale Borussia Dortmund."

Flick aliongeza: "Ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa na ana ubora wa kila aina. Na ndio maana unatakiwa tu kutambua kwamba Dortmund wana mchezaji mzuri sana pale."

Sancho amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho 16 kwenye mechi 26 za Ligi Kuu Bundesliga msimu huu.

# Mbappe: Sina haraka na Ballon d'Or

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe angependa kushinda Ballon d'Or, lakini sio kitu ambacho kinamkosesha usingizi.

Mbappe mwenye umri wa miaka 21, anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora na mshindi wa baadaye wa tuzo hiyo binafsi kwa mchezaji.

Lakini Ballon d'Or imekuwa ikitawaliwa na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, ambao wote kwa pamoja wameshinda mara 11 kati yao tangu mwaka 2008.

Mbappe amesema ni tuzo ambayo angependa kushinda siku moja, lakini hana haraka ya kuitwaa.

"Litakuwa jambo jema kuitwaa, lakini si kitu ambacho kinanipa presha au kunikosesha usingizi usiku," amesema mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa akiliambia gazeti la Mirror.

"Sidhani kama natakiwa kushinda msimu ujao au mwingine unaofuata. Hakuna muda maalumu wa kusema natakiwa kuitwaa.

"Mara zote nitaiweka PSG na timu ya taifa kama kipaumbele changu, halafu kama kuna tuzo binafsi inakuja kwa kutokana na kiwango changu ni kama nyongeza tu."

Katika umri wa miaka 21, Mbappe tayari ameshinda mataji manne ya Ligue 1 na Kombe la Dunia.

Lakini bado hajashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na ndio taji analotaka kulibeba pale PSG.

"Nimepata mafanikio na timu ya taifa, sasa nataka mafanikio ya Ulaya nikiwa na klabu na hayo ndio malengo yangu makubwa," amesema Mbappe.

"Malengo yangu ni kushinda taji la Ulaya nikiwa na PSG na litakuwa jambo la aina yake kwa upande wangu."



HABARI MICHEZO

# Solskjaer anataka Ighalo abaki Man United

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amekubali Manchester United wanaweza kumkosa mshambuliaji anayecheza kwa mkopo hapo, Odion Ighalo mwishoni mwa wiki hii.


United wanajaribu kutaka kuongeza muda wa kubakia hapo Old Trafford wa mchezaji huyo wa zamani wa Watford, lakini hakuna mazungumzo yaliyofanyika na klabu 'mama' ya Ighalo, Shanghai Shenhua ya nchini China.

Kocha Solskjaer anataka kumbakisha Ighalo kwa ajili ya msimu wa ligi utakaporudi tena, baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia wiki za kwanza tangu kutua hapo United.

Muda unakimbia, huku mkataba wa muda mfupi wa Ighalo ukielekea ukingoni ambao walikubaliana Januari, na utamalizika Jumatatu ijayo mwisho wa mwezi huu. Solskjaer ameiambia MUTV: "Mkataba wa mkopo utamalizika mwishoni mwa Mei, hivyo kwa vyovyote atarudi katika klabu yake.

"Tupo kwenye majadiliano. Tunataka abakie hapa, aendelee kucheza katika klabu ya ndoto yake tangu utotoni.

Mchezaji huyo raia wa Nigeria, Ighalo mwenye umri wa miaka 30, ni shabiki wa timu hiyo tangu akiwa mtoto na ameifungia mabao manne katika mechi nane alizoichezea, akifunga katika mara zote tatu alizoanza.






# HENDERSON: HAINOGI KOMBE BILA MASHABIKI

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Jordan Henderson amekubali kwamba litakuwa "jambo geni sana" kunyanyua taji la Ligi Kuu England bila mahudhurio ya mashabiki.

Vijana hao wa Jurgen Klopp wapo kwenye nafasi ya kushinda taji la ligi hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990, wakiwa wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 25 kabla ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Huku ligi hiyo ikiripotiwa kwamba inatarajiwa kurudi tena mwezi Juni lakini bila mashabiki uwanjani, Henderson anaweza kunyanyua taji hilo bila mashabiki wakimwangalia wakiwa benchi.

Kiungo hiyo amesema litakuwa jambo la ajabu kwao, ingawa alionya timu yake bado ina kazi ngumu ya kufanya.

"Bila shaka kutakuwa na hisia tofauti kabisa kwa sababu kama unashinda taji mbele ya mashabiki wako wakiwa pale, inafurahisha sana, hakika litakuwa jambo geni kwetu," amesema Henderson akiiambia BBC Radio 5 Live.

"Mambo hayajaisha bado. Bado tuna kazi ngumu ya kufanya na bado tunahitaji kucheza kwa kiwango chetu cha juu hadi msimu unapomalizika, kwa sababu tunataka kumaliza tukiwa timu imara na yenye nguvu."

# *Pep Guardiola kocha bora duniani, asema Robben*

**MANCHESTER,** England

ARJEN Robben amemwelezea bosi wa zamani wa Bayern Munich, Pep Guardiola kama "mtaalamu wa soka la kuvutia" na amesema mzaliwa huyo wa Katalunya ni kocha bora duniani.

Mchezaji wa zamani wa Uholanzi, Robben ambaye alitangaza kustaafu soka Julai mwaka jana, alitumia misimu mitatu akicheza chini ya Guardiola wakati wa kipindi chake cha mwongo mmoja pale Bayern.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alinunuliwa hapo Bavaria na Louis van Gaal na pia alifanya kazi na Carlo Ancelotti, Jupp Heynckes na Niko Kovac kwa nyakati tofauti pale kwenye dimba la Allianz Arena, pamoja na kuwa chini ya Jose Mourinho kule Chelsea.

Lakini Robben anahisi Guardiola ndio kocha aliyemsaidia yeye kuimarika zaidi kipindi alichokuwa chini yake.

"Napenda soka kuliko kitu chochote, soka la kuvutia na Pep ndio 'masta'," amesema akiliambia jarida la Socrates.

"Anapanga vizuri kwenye ushambuliaji, soka la pasi fupi na umiliki wa mpira. Bila shaka, kwa upekee nilipenda hilo. Tulikuwa kwenye kiwango cha aina yake.

"Alinifanya mimi niwe mchezaji niliyekamilika zaidi. Kwa upande wangu, Pep ni kocha bora duniani. Miaka mitatu niliyokaa nae pale Munich kwa uhakika niliifurahia na ilinijenga zaidi."

Robben alijiunga na Bayern kutoka Real Madrid mwaka 2009 na ameshinda mataji 20, likiwamo la kukumbukwa zaidi la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2013 wakati alipofunga bao la ushindi dhidi ya Borussia Dortmund kwenye fainali.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# COUTINHO ATAJWA KUTUA NEWCASTLE

●●● Endapo Waarabu wa Saudia watakamilisha mchakato wa kuimiliki klabu hiyo baada...

**LONDON,** England

NEWCASTLE United imeanza mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho (28), katika kipindi cha majira ya joto, imeelezwa.

**Mabosi wa Newcastle wamefikia hatua hiyo baada ya Bayern Munich kukosa nafasi ya kumpa mkataba wa kudumu kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Brazil.**

Tayari inaelezwa kiungo huyo Mbrazil alikuwa anajiandaa kurejea Barcelona ifikapo mwishoni mwa Juni mwaka huu baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika Bayern.

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo, Newcastle, ambayo hivi karibuni itakuwa inamilikiwa na kampuni kutoka Saudi Arabia ya PIF, inajiimarisha kumsajili Coutinho na inataka kuona inafanikisha mchakato huo.

Inaonekana huduma ya Coutinho inawindwa na klabu mbalimbani, baadhi yake ni pamoja na Manchester United, Chelsea na Arsenal.

Taarifa zinaeleza kuwa thamani ya kiungo huyo ambaye ni mali ya Barcelona ni pauni milioni 71.

Kwa sasa Coutinho anasumbuliwa na maumivu ya kifundo cha mguu, hiyo inamaanisha kwamba Mbrazil huyo hataweza kushuka dimbani kumalizia mechi zilizobaki za msimu huu.

Kama Newcastle itapokea kibindoni kiasi cha pauni milioni 300, uwekezaji huo utasaidia kuimarisha kikosi cha timu hiyo na usajili wa Coutinho unatajwa kukamilika kwa sababu wanaamini atasaidia timu hiyo kutokana na kuwa na uzoefu kwenye Ligi Kuu England.

Msimu huu, Coutinho amepachika wavuni mabao nane na ametoa pasi za mwisho sita kwenye michezo 22 aliyocheza ya Bundesliga.

Coutinho alijiunga na Barcelona Januari mwaka 2018 akitokea Liverpool, lakini alishindwa kupambana na kupata namba ya kudumu katika kikosi cha Nou Camp, mkataba wake na klabu hiyo utamalizika kwenye majira ya joto 2023.

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE YAMTAJA SHAQIRI

MABOSI wa Newcastle United wametangaza nia ya kumsajili kiungo wa Liverpool, Xherdan Shaqiri ambaye ana umri wa miaka 28, ifikapo majira ya joto. Mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Uswisi ameichezea Liverpool mechi 10 tu msimu huu. ***(Mail)***

### WAARABU MATATANI

KAMPUNI ya Waarabu wa Saudi Arabia ambao wanataka kuinunua Newcastle kwa dau la pauni milioni 300 huenda wakakwama kukamilisha mchakato huo baada ya Soko la Biashara la Dunia kubaini nchi yao iko nyuma ya kampuni moja ambayo huenda ikahujumu kwa kutoa huduma ya televisheni kinyume na taratibu. ***(Guardian)***

### ARSENAL, SPURS VITANI

ARSENAL na Tottenham zote zinapambana kuwania saini ya kiungo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Brazil, Willian (31), ambaye anatarajia kuwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wa kuitumikia klabu hiyo ya Stamford Bridge ifikapo majira ya joto. ***(Telegraph)***

### PALHINHA ANUKIA WOLVES

WOLVES inajipanga kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon Mreno Joao Palhinha, ambaye ana umri wa miaka 24, na dau lake limetajwa kuwa ni pauni milioni 18. ***(Mirror)***

### HANSEN ANUKIA CITY

MANCHESTER City inaongoza katika mbio za kuwania saini ya mshambuliaji chipukizi wa Ajax, Sontje Hansen (18), ambaye alishinda kiatu cha dhahabu kwenye fainali za Kombe la Dunia la vijana wa umri chini ya miaka 17 (U-17), zilizofanyika mwaka jana. ***(Goal)***

### RAYMOND SOKONI

KLABU ya Vitoria Guimaraes ya Ureno inajiandaa kumsajili kiungo wa Crystal Palace, Jadan Raymond (16), kwa dau la pauni 250,000. Mkataba wa chipukizi huyo unatarajiwa kumalizika mwezi ujao. ***(Sky Sports)***

### KLABU EPL ZAJIPANGA

KLABU za Ligi Kuu England zinajiandaa kusaka njia mbadala ya kisasa ya kupata mashabiki wanaoingia viwanjani mara ligi hiyo itakaporejea huku milango ikiwa imefungwa, ikiwamo kwa kutumia mfumo wa matangazo wa LED kwenye mabango ya televisheni. ***(Express)***

### PELLEGRINI AGOMBEWA

PARIS Saint-Germain inajiandaa kunasa saini ya kiungo wa AS Roma na Timu ya Taifa ya Italia, Lorenzo Pellegrini. Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo anatajwa kuwa shabiki mkubwa wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23 ambaye anawindwa na Juventus, AC Milan na Everton. ***(Soccernet)***

### CASEMIRO KUBAKIA MADRID

NYOTA Casemiro anatajwa hataondoka Real Madrid katika siku za hivi karibuni. Kiungo huyo alisaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo ya Bernabeu hadi mwaka 2023. ***(Marca)***

### TEVEZ ATAKIWA BOCA

RAIS wa Boca Juniors, Jorge Ameal anaamini mshambuliaji, Carlos Tevez (36), ataendelea kuitumikia klabu hiyo kwa msimu mwingine baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika ifikapo Juni 30, mwaka huu. ***(Mail)***

# YANGA YAISHTUKIA AZAM FC LIGI KUU

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema umeamua kuanza mazoezi ya pamoja mapema zaidi kwa sababu ya kutimiza malengo yao ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Awali Yanga ilitangaza kuanza mazoezi ifikapo Juni Mosi, mwaka huu, lakini klabu hiyo iliamua kuwaita kambini wachezaji wake juzi na kuendelea kujiwinda.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema wanaimani wachezaji wanatakiwa kupata muda mwingi wa mazoezi kwa ajili ya kuimarisha miili yao na kuwa tayari na mapambano.

Mwakalebela alisema tayari wachezaji wao wameshafanya vipimo vya afya pamoja na kushiriki semina maalumu iliyoandaliwa ili kupata elimu ya kujilinda na virusi vya ugonjwa wa corona.

"Tayari tumeanza zoezi endelevu la kuwapokea wachezaji wetu pamoja na kuwafanyia vipimo, walianza kuwasili jana (juzi) na leo (jana), wataanza kazi rasmi ya mazoezi chini ya Kocha Msaidizi, Charles Mkwassa," alisema Mwakalebela.

Aliongeza kila mchezaji wa Yanga yupo tayari kuendeleza 'mapambano' kwa ajili ya timu hiyo kuondoka na ushindi kwenye mechi zote zilizobakia na vile vile kubakia na afya salama.

Kiongozi huyo alisema bado wanaendelea kufuatilia utaratibu wa safari kwa ajili ya kurejea nchini golikipa wao, Farouk Shikalo ambaye bado mpaka wa Tanzania na Kenya haujafunguliwa.

"Suala la Shikalo lipo nje ya uwezo wetu, ila tunapambana kuhakikisha mchezaji huyo anarejea kwa wakati na kuwahi kabla ya ligi haijaanza rasmi," alisema Mwakalebela.

Yanga yenye pointi 51 na iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, imebakisha michezo 11 ili kumaliza msimu huu wa 2019/20 wakati mabingwa watetezi ni Simba na inaongoza ligi ikiwa na pointi 71.



Kocha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije (katikati), akiwa na wachezaji wa klabu mbalimbali za Ligi Kuu Bara baada ya kumaliza mazoezi kwenye ufukwe wa Escape One jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

## Ligi Kuu Zanzibar kuendelea Juni 5

**Na Hawa Abdallah**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza kuwa Ligi Kuu ya visiwani humo itarejea tena kuwania Juni 5, mwaka huu.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema jana Ligi Kuu pekee ndio itakayorejea na michezo mingine itaendelea kusubiri hadi hapo serikali itakapotoa taarifa nyingine.

Hata hivyo, Balozi Iddi alisema kuwa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) na Wizara ya Afya zitatakiwa kukutana ili kuandaa mwongozo bora wa kuendesha ligi hiyo.

Kiongozi huyo alisema kwa sasa michezo mingine inayohusisha vikundi au makundi ya wananchi ikiwamo mazoezi ya uwanjani na ufukweni hayataruhusiwa kufanyika.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Haji Issa Kidali, alisema wamepokea agizo hilo la kuendelea kwa ligi na watatoa wiki mbili za kufanya mazoezi kwa kufuta kanuni zote za afya.

Kidali alisema baada ya wizara hizo mbili husika zitakapowapatia mwongozo, watatangaza ratiba kamili ya ligi hiyo ya juu Zanzibar.

## Serikali yaviita vyama mezani

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo Taifa (BMT), limetoa wito kwa vyama vya michezo kupeleka programu na mikakati yao kwa ajili ya kufungua 'mlango' wa majadiliano.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mkuu wa BMT, Neema Msitha, alisema wanahitaji kupokea mikakati kutoka kwa wadau wao ili kujadiliana kabla ya kuanza kwa michezo mbalimbali baada ya kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa wa corona.

Msitha alisema BMT ilianza kukutana mara kwa mara na viongozi wa soka na kupokea programu na mapendekezo yao kuhusiana na namna watakavyorejea kumaliza msimu katika kipindi hiki cha kupambana na corona.

"Baada ya baraza kupokea taarifa ya mipango kutoka kwa wadau wake, kutakuwa na majadiliano ya pamoja kwa kushirikiana na wataalamu kutoka katika Wizara ya Afya na vyama husika ili kupata mwongozo wa utekelezaji wa programu hizo kwa kuzingatia tahadhari," alisema Msitha.

Alisema corona bado ipo na wananchi wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari ya kujiepusha na maambukizo wakati wakirejea kwenye michezo yao.

Rais Dk. John Pombe Magufuli alitangaza kufungulia michezo yote kuanzia Juni Mosi, mwaka huu kwa kutambua michezo ni burudani na inasaidia kuimarisha kinga za mwili.

## Selem View FC yalalamikia ratiba

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Selem View, Ali Khalid, amesema sababu iliyochangia timu yake kufanya vibaya katika Ligi Kuu Zanzibar msimu huu ni kuwapo kwa 'pangua pangua' ya ligi hiyo iliyotokana na changamoto ya fedha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Khalid alisema kauli hiyo iliweza 'kuwatoa mchezoni' wachezaji wake na kuondoa hali ya hamasa iliyokuwapo kwenye kikosi chake. Khalid alisema hali ya sintofahamu ya 'mara kwa mara' kwenye ligi hiyo, ilisababisha pia wachezaji wake kutokuwa na morali ya kusaka matokeo mazuri wakati ligi hiyo ilipokuwa inaendelea.

"Awali tulikuwa katika nafasi nzuri, kuna wakati kwenye msimamo tulikaa katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa timu 16," alisema kocha huyo.

Aliongeza pia kusimama kwa ligi hiyo kwa ajili ya kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), iliyokwenda kwenye michuano ya Chalenji mwaka jana ambayo ilifuatana na dirisha dogo la usajili.

"Kwa upande wangu, suala la usajili wa wachezaji sio sababu kubwa ya kufanya vibaya kwa kuwa timu zote za Zanzibar usajili wao hautofautiani, ila kitendo cha kusimamisha ligi mara mbili, na hata zile kauli za ligi itasimama iliwavunja moyo wachezaji kuendelea kujituma, kumbuka na hali ya umaskini wa timu zetu," Khalid alisema.

Selem View yenye maskani yake Pemba, ina pointi 17, iko nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

Michezo

Alhamisi Mei 28, 2020

Nipashe



Coutinho atajwa kutua Newcastle UKURASA 22



Daktari wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Yassin Gembe (kushoto), akimfanyia vipimo beki wa timu hiyo, Gadiel Michael baada ya kuwasili kwenye kambi ya timu hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SIMBA**

# KAGERE KUPEWA 'DOZI' MAALUMU

## ●●● Lengo ni kuvunja rekodi ya kupachika mabao inayoshikiliwa na Mmachinga Ligi Kuu...

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha anarejea kwenye makali yake na kufikia rekodi iliyowekwa na Mohammed Hussein 'Mmachinga', benchi la ufundi la mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, limemwandalia programu maalumu mshambuliaji wao, Meddie Kagere.

**Kagere alirejea nchini juzi akitokea kwao Rwanda baada ya kupata kibali maalumu cha kuripoti kwenye kituo chake cha kazi kutoka kwa Serikali ya Rwanda.**

Kagere ana mabao 19 na anaongoza katika orodha ya wafungaji, huku Mmachinga aliyefunga magoli 26, bado rekodi yake haijavunjwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema lengo la kumwandalia mazoezi tofauti mshambuliaji huyo ni kwa sababu wanataka afikie rekodi iliyokuwa inashikiliwa na Mmachinga kwenye ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

Matola alisema wanamwandaa vizuri mshambuliaji huyo ili afunge mabao mengi zaidi katika michezo 10 iliyobakia na hatimaye kutimiza malengo ya timu yake katika kupata tuzo hiyo.

Nahodha na kiungo huyo wa zamani wa vinara hao wa Ligi Kuu Bara alisema anaimani mshambuliaji huyo anaweza kufunga bao katika kila mechi atakayocheza na hatimaye kufikia au kuvunja rekodi hiyo iliyodumu kwa muda mrefu hapa nchini.

"Leo (jana) tumeanza mazoezi rasmi, akiwamo Kagere ambaye amerejea na sasa tunajipanga kumsaidia kiufundi katika suala la kuvunja rekodi ya kufunga mabao mengi," alisema Matola.

Kocha huyo alisema kwa sasa wanachohitaji ni kuona Mnyarwanda huyo anavunja rekodi sambamba na timu ikitwaa ubingwa kwa mara tatu mfululizo.

"Suala la ubingwa kwetu halina pingamizi, kwa sababu tunaasilimia kubwa ya kutetea taji hilo, hivyo tunahitaji kushinda mechi nne tu ili tupate pointi ambazo hazitoweza kufikiwa na wengine," alisema Matola.

Mbali na vita ya kuwania taji la Ligi Kuu, Simba bado iko kwenye michuano ya Kombe la FA ambayo imeingia kwenye hatua ya robo fainali na bingwa wake hupata tiketi ya kuiwakilisha Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## Mbivu na mbichi za Mwamnyeto

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya tetesi za muda mrefu za beki wa Coastal Union na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Bakari Mwamnyeto kuwindwa na vigogo wa soka nchini, meneja wa mchezaji huyo, Kassa Mussa, ameibuka na kusema Yanga ndiyo imefanya rasmi mazungumzo naye.

Kassa aliliambia gazeti hili kuwa Yanga ndiyo klabu pekee iliyofanya mawasiliano naye kumwania beki huyo ambaye bado ana mkataba wa mwaka mmoja na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara mwaka 1988.

Meneja huyo alisema mazungumzo hayo yanaendelea na yanamhusisha Mwamnyeto, Coastal Union na Yanga ambayo inahitaji huduma ya mchezaji husika.

"Yanga wameonyesha nia ya dhati, lakini bado hatujafikia muafaka, tunasubiri kuona mwisho wake, ingawa Simba pia wameonyesha nia japo hawajafanya mazungumzo nasi," alisema Kassa.

Hata hivyo meneja huyo hakuwa tayari kuweka hadharani dau ambalo wameitaka Yanga itoe ili kunasa saini ya mlinzi huyo na kueleza kiasi hicho ni siri kwa pande hizo tatu ambazo ziko kwenye mazungumzo.

## Mwalusako aagwa, kuzikwa leo Kyela

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA beki tegemeo wa Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Lawrence Mwalusako, anatarajiwa kuzikwa leo kijijini kwao Kyela, Mbeya, imeelezwa.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela alisema kuwa wanachama, mashabiki wa Yanga na wadau wengine wa michezo walijumuika kutoa salamu za mwisho za marehemu Mwalusako jana nyumbani kwake Ubungo, jijini Dar es Salaam.

"Baada ya kumaliza tukio la kumuaga hapa nyumbani, leo (jana) tutausafirisha mwili wa marehemu kuelekea Mbeya na kesho (leo), tutamzika katika kijiji cha Kyela, " alisema kwa kifupi Mwakalebela.

Enzi za uhai wake, Mwalusako ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Yanga aliwahi kuichezea kwa mafanikio Pan African.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >